Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Pili - Tarehe 9 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 11

**Hospitali ya *Sekou-Toure* Jijini Mwanza**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya *Sekou Toure* Jijini Mwanza imejengwa kwa nguvu za wananchi ili kuiboresha kuwa kwenye hadhi ya Hospitali ya Mkoa:-

(a) Je, mpaka sasa Serikali imetoa fedha kiasi gani kama mchango wake kwenye ujenzi huo?

(b) Je, Serikali ina majukumu gani kwenye ujenzi wa Hospitali za Mikoa ambazo ni shughuli muhimu inazozitambua?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen M. Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 1988, Kamati ya Maendeleo ya Mkoa wa Mwanza iliamua kupanua Kituo chake cha Afya cha *Sekou-Toure* kilichopo Kata ya Isamilo, Jijini Mwanza, kuwa Hospitali ya Mkoa baada ya kukamilisha taratibu zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kupata kibali cha Wizara ya Afya. Kazi ya upanuzi wa kituo hicho kuwa Hospitali ya Mkoa ilianza mara moja na ilipofika mwaka 1994 ilianza kufanya kazi kama Hospitali ya Mkoa. Aidha, tangu uamuzi huo uchukuliwe mpaka sasa Serikali imeweza kujenga wodi ya wanawake, wodi ya wanaume, wodi ya watoto, wodi

ya wazazi, wodi ya malipo *(Private)*, jengo la wodi ya upasuaji na jengo la jiko. Serikali pia imeweza kujenga jengo la ufuaji na la kuhifadhi maiti, imekarabati majengo ya zamani na kununua gari la wagonjwa, friji ya *mortuary* na *X-ray.*

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha kazi nilizozielezea, Serikali imechangia jumla ya Sh. 772,219,685/=. Fedha hizo zimetokana na ruzuku ya Serikali pamoja na mkopo wa Benki ya Dunia kupitia Programu ya Mfuko wa Afya inayosimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mchango wa wananchi katika upanuzi wa Hospitali ya *SekouToure* ni Sh. 250,000,000/=. Aidha, ili kuharakisha kazi ya upanuzi wa Hospitali ya *Sekou Toure,* uongozi wa Mkoa uliunda Kamati ya uhamasishaji iliyozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, tarehe 13 Oktoba, 2003 na katika uzinduzi huo Mheshimiwa Rais alichangia Sh. 1,000,000/=. Mheshimiwa Mbunge wa Mwanza Mjini ni Mjumbe wa Kamati niliyoitaja na nina imani kwamba na yeye mwenyewe ameshachangia.

(b) Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali katika ujenzi wa Hospitali za Mkoa ni pamoja na kubuni na kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya ujenzi/upanuzi wa hospitali hizo, kuhamasisha jamii kuona kwamba ujenzi ni wetu sote na hivyo kuchangia, kusimamia shughuli za upanuzi wa Hospitali na kuhakikisha kuwa hospitali inapatiwa madawa na watumishi wanaohitajika.

Shughuli za upanuzi wa Hospitali ya Mkoa Mwanza zinatarajiwa kumalizika ifikapo Oktoba, 2005. Napenda kutoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Mwanza, akiwemo Mheshimiwa Mbunge, kujitokeza kutoa michango kwa wingi ili kukamilisha upanuzi wa Hospitali ya Mkoa wao.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kazi inayoendelea sasa ya upanuzi wa hospitali ili kuiboresha ni kubwa na inaelekea kugharimu zaidi ya shilingi bilioni moja nukta nane na kilio chetu ni kutaka Serikali iungane na wananchi kwenye kazi hii na nilitegemea leo Wizara au Serikali ingeweza kusema kwamba, itasimamia na kusimamisha jengo la maabara au *general ward* ambazo ni *ward* kubwa na zenye pesa nyingi sana. Sasa swali, je, Serikali kwa leo itatamka itafanya nini kwenye hospitali hii ya Mwanza? *(Makofi)*

Pili, kama msimamo ni kwamba wananchi wa Mwanza waendelee kuchangia pamoja na kwamba wanalipa kodi zote, je, Serikali au Wizara itasaidiana vipi na watu wa Mwanza katika ku-*raise funds* zaidi kwenye ujenzi wa hospitali hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, ujenzi wa hospitali hii utakamilika ifikapo Oktoba, 2005. Hiyo ni pamoja na michango ya wananchi na michango itakayotoka Serikalini. Programu iliyowekwa ni hiyo na kama tunavyofahamu, utekelezaji wa programu hizi unategemea kupatikana kwa fedha, Serikali imeweka kwenye programu kwamba itakamilika mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sehemu ya pili ya swali lake, napenda kusema kwamba, Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi katika kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, swali langu ni kwamba, kwa kuwa kazi zinazofanywa na nguvu za wananchi zinakuwa ni nyingi karibu nchi nzima na michango hii inahusisha kodi mbalimbali. Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka kwa miradi kama hii ya ujenzi wa Hospitali ya *Sekou Toure* na ujenzi wa madarasa au shughuli ambazo zinahusisha umma moja kwa moja zikasamehewa kodi zinazohusiana na ununuzi wa vifaa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kodi zinazotozwa na Serikali ni kama zinavyopitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na swali linalofuata, napenda kuwatambulisha wageni wa Kimataifa waliopo katika *Gallery* ya Bunge leo asubuhi, ambao ni maafisa wawili kutoka Bunge la Uingereza *(House of Commons),* ambao wamekuja kuungana na wataalam wetu kutusaidia katika mipango yetu ya *capacity building. I wish to introduce visiting officers from the House of Commons, London, you are welcome today. (Makofi)*

Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Omar Mwenda.

Na. 12

**Huduma za Afya Kilwa Kusini**

**MHE. OMAR M. MWENDA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Tarafa ya Pande ni wengi sana na wanategemea kupata huduma katika Kituo cha Afya kilichopo Tarafani na kwa kuwa akinamama wajawazito wakishindwa kujifungua hupelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kilwa Kivinje kwa kutumia usafiri wa majini kwa mwendo wa kilomita 28 hadi Kilwa Masoko na kutoka Kilwa Masoko hadi Kilwa Kivinje ni kilomita 29 na kwa kutumia njia ya barabara bila kupita majini kwa umbali wote ni kilomita 128 na hakuna chombo cha aina yoyote cha usafiri yaani boti wala gari:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa wakati umefika sasa wa kupanua kituo hicho cha Afya kuwa Hospitali yenye uwezo wa kutoa huduma zaidi ikiwemo huduma ya upasuaji?

(b) Kwa kuwa vituo vyote vya afya hupatiwa usafiri, je, Serikali iko tayari kukipatia kituo hicho usafiri wa kuaminika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, Tarafa ya Pande ina wakazi 38,905 wanaoishi katika Kata za Pande, Mandawa, Lihimaliyao na Kiranjeranje. Wilaya ya Kilwa ina jumla ya wakazi 171,850. Kulingana na Sera ya Afya, vigezo vinavyoangaliwa kabla ya kuanzisha Vituo vya huduma za afya ni idadi ya wakazi, kuwepo kwa wataalam na vifaa. Kwa kuzingatia vigezo hivyo, zahanati inatakiwa kuhudumia wakazi wasiopungua 10,000, Kituo cha Afya kinahudumia wakazi 50,000 na Hospitali inatakiwa kuhudumia wakazi 100,000. Kwa misingi ya vigezo hivi, Kituo cha Afya cha Pande, hakistahili kupewa hadhi ya Hospitali kutokana na idadi ndogo ya wakazi inayowahudumia ambayo haikidhi hata kuwa Kituo cha Afya.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Pande. Tayari Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imepokea Sh. 45,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa gari hilo. Hivi sasa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa unakamilisha taratibu za ununuzi wa gari hilo kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi. Aidha, ili kurahisisha mawasiliano, Kituo hiki kina simu ya upepo *(Radio Call).*

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa kuweza kunipatia usafiri huo wa gari, lakini pamoja na hayo naomba niulize swali moja dogo. Kwa kuwa eneo letu kifuku barabara haipitiki pamoja na kupata gari bado tatizo lipo, je, wananchi hawa waendelee kufa kwa vile hawajatimia hamsini elfu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli lipo tatizo la usafiri lakini gari la wagonjwa tulilolitoa ni kwa ajili ya barabara, sasa kama barabara hazipitiki wakati wa kifuku, basi wananchi na Serikali yao, tutaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba barabara hizo zinapitika.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na napenda niulize swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa takwimu ambazo sasa hivi zinatumika kwa kituo cha afya wanahitaji watu 50,000 na zahanati ni elfu nne au tano, ambazo zimepitwa na wakati ukilinganisha na takwimu za ulimwengu. Je, sasa isingekuwa vizuri Serikali ikaangalia upya kwa sababu ya utandawazi na hali ya afya za wananchi iweze kurekebisha takwimu hizi ili wananchi waweze kujenga zahanati na hospitali kwa wingi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli inawezekana takwimu zimepitwa

na wakati, lakini vile vile tunajua kwamba, unaweza kujenga majengo lakini kama huna waganga na huna vifaa, majengo hayo hayatatumika kama hospitali. Kwa hiyo, hayo yanafuatana na uwezo wetu, tukiwa na waganga wa kutosha na vifaa vya kutosha, naamini kwamba tunaweza kuteremsha takwimu hizo. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubaliana na kifungu (b) cha swali la msingi na Mheshimiwa Waziri anajua kwamba kwa muda wa miaka mingi nilikuwa nikiomba Serikali iweze kuvipatia magari Vituo vya Afya vya Mwanarumango na Mzenga lakini havikupata. Je, hivi sasa yupo tayari kupeleka magari katika vituo hivyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli bado tunahitaji kuongeza huduma katika vituo vyetu vya afya lakini kama nilivyosema hili linategemea uwezo wa Serikali. Jinsi tunavyopata wataalam na uwezo wetu wa kifedha unavyoongezeka, basi naamini kwamba tutaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge.

Na 13

**Barabara ya Mutukula - Muhutwe**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa ujenzi wa barabara ya lami ya Mutukula - Muhutwe kulifanyika tathmini ya mali za watu zilizokuwa zimeathiriwa na eneo lililopimwa kujengwa barabara na fidia kulipwa kwa wahusika na kwa kuwa kufuatana na vipimo halisi vinavyotakiwa kisheria kwa maeneo au mali ambayo haikufidiwa wakati wa ujenzi wa barabara hiyo iliyojengwa:-

(a) Je, kuna mpango gani wa Serikali kulipa fidia kwa mali iliyomo katika eneo ambalo lilikuwa halijafidiwa?

(b) Kwa kuwa mara nyingi watendaji wa Serikali huwa na kawaida ya kutangulia kuweka alama ya "X" bila majadiliano wala muafaka wa wenye mali ikiwa ni kuashiria hatari inayokuja ya kumbomolea mtu mali wakitangaza hali ya hatari hiyo inaweza kusababisha kuvunja amani?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwaelewesha wananchi juu ya zoezi hilo kwa maeneo husika kabla ya kuweka alama hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fidia ya nyumba, mazao na mali nyingine zilizokuwemo ndani ya eneo la ujenzi *(Construction Corridor)* kwenye mwelekeo mpya *(New Alignment)* wa barabara ya Mutukula - Bukoba - Muhutwe ambayo ina urefu wa kilomita 112 ilifanyika katika upana wa mita 30 badala ya mita 45 ambao ndio upana wa hifadhi ya barabara kisheria ili kupunguza gharama ya fidia. Ujenzi wa barabara ulihitaji eneo la mita 30, mita 15 kila upande kutoka katikati ya barabara mpya iliyobuniwa wakati wa usanifu wa barabara hii. Katika zoezi linaloendelea la kuweka alama ya "X" kwenye nyumba au mali zilizomo kwenye eneo la hifadhi ya barabara katika Mkoa mzima wa Kagera na Mikoa mingine nchini, nyumba au mali zilizomo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara yenye upana wa mita 45 zimeorodheshwa na kuwekwa alama za "X" ili kuzitambua na pia kuwatahadharisha wananchi wasivamie kulima mazao ama kujenga nyumba mpya ndani ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utangulizi hapo juu, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ina mpango wa kulipa fidia eneo la mita 15 lililobaki na linalostahili fidia kwenye mwelekeo mpya wa barabara pindi fedha zitakapopatikana. Aidha, Serikali haitafidia nyumba na mali zilizomo kwenye eneo la mita 30 ambalo limeshafidiwa na zile ambazo zimejengwa baada ya kulipa fidia katika eneo ambalo halikufidiwa la mita 15.

(b) Wakati wa kuweka alama za "X" kwenye mali zilizopo ndani ya hifadhi ya barabara, Serikali inashirikiana na viongozi wa maeneo husika kuwajulisha wananchi kuhusu zoezi hili. Aidha, ijulikane kuwa kujenga ndani ya eneo la hifadhi ya barabara bila kibali cha Wizara ni kukiuka Sheria ya Barabara *No. CAP 167* ya mwaka 1967, hivyo Serikali hailazimiki kuwa na muafaka na wananchi wakati wa kuweka alama za "X". Lakini kwa kutumia uungwana na ubinadamu, Serikali huwahusisha viongozi wa ngazi zote.

(c) Wizara inafanya jitihada kuhakikisha kuwa wananchi wanaelimishwa na kuhamasishwa kiasi cha kutosha kuhusu suala hili ili kuondoa hofu na wasiwasi kwa wananchi. Vile vile Wizara inaendesha vipindi katika Redio na kuchapisha maelezo kwenye magazeti mbalimbali hapa nchini hususan ya Kiswahili ikiwa ni mpango mahsusi *(strategy)* wa kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria na kanuni za hifadhi ya barabara.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba kujua kwamba Serikali inatamka nini kuhusiana na fidia kwa watu ambao walijenga kwenye *corridor* ya barabara na kufanya makazi yao ya kudumu kabla Sheria hii ya mwaka 1967 kutungwa?

Pili, kumekuwa na kauli mbalimbali ambazo kidogo zinatofautiana kutoka upande wa Serikali. Kauli mojawapo ikiwa ni kwamba watu waliojenga kwenye *corridor* watake wasitake hata kama wapo tayari kukinyima Chama fulani kura, hizo nyumba

zitabomolewa na kauli nyingine ni kwamba Serikali imeona huruma na kwamba imeahirisha zoezi hilo mpaka wakati mwingine muafaka. Sasa ningeomba kupitia Bunge hili wakati muafaka huo ni upi, isije ikawa ni baada ya mwaka 2005 baada ya uchaguzi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Hifadhi ya Barabara ya Mwaka 1967 ilikuwa *reviewed* mwaka huo, lakini sheria hii imeanza mwaka 1932, ikaja kuwa *reviewed* Bungeni mwaka 1947, ikaja kuwa *reviewed* Bungeni mwaka 1967 na ndiyo tunayoitumia. Kwa hiyo, aliyekuwepo kabla ya mwaka 1932 ndiye mwenye haki ya kudai. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kauli mbalimbali za msimamo wa Serikali. Baada ya kuombwa kutoa tamko rasmi la msimamo huu, Waziri wa Ujenzi, alitayarisha tamko na tukaitisha *press conference* na tukatoa msimamo rasmi wa Serikali na naomba niurudie kwa ufupi. Tunatia alama za "X" kwenye hifadhi ya barabara ili kuwajulisha wananchi kwamba wamo kwenye hifadhi hiyo. Pale ambapo Serikali haina pesa ya kujenga barabara hiyo, wananchi wanahama polepole, tutakapopata pesa tutahusisha viongozi wafuatao kabla hatujawaambia wabomoe na Serikali sasa haibomoi nyumba, wanawaomba wananchi wenyewe wabomoe kwa sababu Serikali ikibomoa nyumba maana yake gharama ya tingatinga, huyu mwenye nyumba lazima alipe na sisi tunaona si vizuri.

Sasa msimamo ni kwamba, tukipata pesa Mwenyekiti wa Kijiji, Diwani na Mbunge, watahusika katika barabara hiyo, kutoa taarifa rasmi kama Mbunge hutaki kuja sisi tutakwenda lakini tutakupa taarifa kwamba, sasa tumepata pesa za kutengeneza barabara hii na wananchi ambao wapo kwenye hifadhi za Serikali waende pembeni tutengeneze barabara hii. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 14

**Mpango wa Maendeleo wa Kanda ya Mtwara**

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI (k.n.y. MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME)** aliuliza:-

Kwa kuwa upo Mpango wa Maendeleo wa Kanda ya Mtwara na kwa kuwa mpango huo kama utakamilika yapo matumaini makubwa ya kuinua hali ya maendeleo ya Kanda hiyo ambayo yamedumaa kwa ajili ya kukosekana kwa miundombinu:-

(a) Je, ni mambo gani ambayo yametekelezwa tangu mpango huo uanze?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza ni mambo gani yanayotegemewa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo?

(c) Je, Serikali inasemaje kuhusu utekelezaji wa mpango huo ambao ndio wenye matumaini ya kuleta maendeleo katika Kanda ya Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, naomba nitoe historia fupi kuhusu Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara kama ifuatavyo:-

Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara *(Mtwara Development Corridor),* ulianzishwa mwaka 1997 kutokana na juhudi za Wakuu wa Nchi za Tanzania, Malawi, Msumbiji na Zambia. Ukanda huu unajumuisha maeneo yafuatayo kwa nchi zote wanachama:-

- Tanzania: Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa na maeneo yaliyo kusini mwa Mto Rufiji katika Mikoa ya Pwani na Morogoro.

- Malawi: Mikoa ya Kaskazini na Kati.

- Msumbiji: Majimbo ya Cabo Delgado na Niassa.
- Zambia: Majimbo ya Kaskazini na Mashariki.

Maeneo hayo ndiyo yanafanya *Mtwara Corridor.*

Madhumuni ya kuanzisha ukanda wa Maendeleo wa Mtwara yamelenga kuongeza kasi ya maendeleo katika maeneo haya kwa kushirikiana na kuanzisha kwa pamoja miradi mbalimbali ya kiuchumi katika nchi zote wanachama. Lengo kuu ni kuwezesha matumizi ya raslimali zilizomo katika maeneo haya ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi ya wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ufafanuzi kuhusu historia fupi ya Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi sasa mambo muhimu ambayo yametekelezwa tangu kuanzishwa kwa mpango huu ni yafuatayo:-

(i) Kuwepo kwa Muundo wa Usimamizi na Uratibu wa *Mtwara Development Corridor,* ambao umekubaliwa na nchi zote wanachama. Muundo huo upo katika ngazi mbili, ngazi ya Kitaifa *(National Level)* na ngazi za kikanda *(Interstate Level).* Aidha, katika ngazi zote mbili, Kamati mbalimbali zimekwishaundwa na nchi wanachama. Kamati hizi zinahusisha Wataalam, Makatibu Wakuu na Mawaziri;

(ii) Kuandaliwa kwa rasimu ya Makubaliano ambapo pindi itakaposainiwa na nchi wanachama itaipa *Mtwara Development Corridor* uhai wa kuwepo kisheria. Mipango ya utiaji saini *Memorandum of Agreement* inaandaliwa ambapo Wakuu wa Nchi Wanachama wataweza kuweka sahihi; na

(iii) Kazi ya kuainisha miradi mbalimbali kwa nchi wanachama inaendelea. Baadhi ya miradi ama maeneo yaliyoainishwa yamelenga kuendeleza miundombinu ikijumuisha barabara, bandari, mawasiliano, viwanja vya ndege na reli. Kukuza uchumi *(Economic Potentials),* ambayo inajumuisha uchimbaji wa madini, nishati, kilimo, maliasili na utalii na kukuza maendeleo ya kijamii ambayo inajumuisha huduma za elimu na afya.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na nchi wanachama, inategemea kutekeleza baadhi ya miradi mikubwa *(Anchor Projects),* ambayo itapewa kipaumbele na nchi wanachama. Inategemewa kuwa utekelezaji wa miradi hii utakuwa ni kichocheo cha kuharakisha maendeleo na kufungua milango katika kuendeleza miradi mingine katika ukanda huu. Kwa upande wa Tanzania, miradi hii inajumuisha miradi ifuatayo: Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Umoja *(Unity Bridge)* litakalounganisha Tanzania na Msumbiji, Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Mtwara - *Mbamba Bay* ambayo itaunganisha Tanzania na Malawi, Mradi wa uzalishaji umeme wa mkaa wa mawe wa Mchuchuma *(Mchuchuma Coal Project),* ambao unatarajiwa kuzalisha megawati 400 za umeme na makubaliano ya kuimarisha Bandari za *Nkhata Bay* na *Mbamba Bay* kwa nchi za Tanzania na Malawi. Aidha, kukamilisha makubaliano ya kisheria *(Memorandum of Agreement)* kuhusu *Mtwara Development Corridor.*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali na itaendelea kufanya jitihada za dhati ili programu hii muhimu ya *Mtwara Development Corridor* itekelezwe kikamilifu. Ni matumaini ya Serikali kwamba, kwa baadhi ya miradi ambayo utekelezaji wake umeshaanza, mara itakapokamilika itafungua mlango wa maendeleo katika ukanda huu.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kutokana na maelezo ambayo yametolewa inaonyesha kana kwamba *Mtwara Corridor* bado ipo katika hali ya kienyeji yaani bado haijawekwa *officially,* ni suala ambalo linazungumzwa tu halijaweza kuwekwa katika utaratibu uliokuwa sawasawa. Kwa hiyo, je, hayo mambo yanayokusudiwa kufanywa katika kipengele (b) yatafanywa namna gani wakati mpango wenyewe haujawa *official?*

Pili, kutokana na hali ambayo tayari *Mtwara Corridor* tangu ianzishwe imepita sasa karibu miaka saba na hakuna jambo muhimu ambalo katika hayo halijafanywa kuwa ni *official.* Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba, sasa umefika wakati suala lenyewe liwekwe katika njia iliyokuwa sawasawa ili mambo yatekelezwe kwa utaratibu unaotakiwa au unaofaa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, *Mtwara Development Corridor* ipo rasmi lakini haipo kisheria. Hiki ni Kiswahili.

**SPIKA:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Ipo rasmi lakini haipo kisheria. Ipo rasmi kwa sababu nchi zote ambazo zinahusika viongozi wake wamekubaliana na wamewaelekeza watendaji wao waendelee na kazi. Lakini kisheria inatakiwa viongozi hao wote watie saini *Memorandum of Agreement.* Ilikuwa tayari itekelezwe mwaka 2003, bahati mbaya kiongozi wetu aliugua wakati hiyo iko tayari. Sasa tunangoja akishakuwa tayari na wenzake wamesharidhika kwamba, akishakuwa tayari wao watakuja hapa kutia saini Mkataba, lakini Mkataba uko tayari. Kuwepo kisheria, lakini kwa sababu ipo tayari rasmi, sisi watendaji tunaendelea kutenda kazi na mojawapo ni haya mambo ambayo nimeyatamka hapa na barabara ya Mtwara mpaka *Mbamba Bay* tayari imeshafanyiwa *feasibility study* na sasa tunaifanyia usanifu. Kwa hiyo, sisi hatungoji huo Mkataba mpaka utiwe saini na uwe sheria. Utakapokuwa kisheria sasa ni masuala ya mikataba ya ujenzi, nani anahusika kwenye mikopo na mambo mengine, hiyo ndiyo maana lazima iwepo kisheria, lakini kuwepo rasmi, ipo tayari rasmi. Nina hakika kabisa kabla ya mwisho wa mwaka huu, itakuwepo kisheria na hivyo ina haki ya mambo mengine yote kuendelea.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu alisahau kusema kwamba, moja ya mambo ya utekelezaji yaliyofanyika ni kuweka alama ya "X" kwenye barabara yote inayotoka Mtwara kwenda hadi Masasi. Lakini swali langu ni kwamba ni fedha kiasi gani kwa Dola au kwa Shilingi zilizotolewa hadi sasa katika tathmini, *feasibility study* na maendeleo yote yanayosemwa yamefikiwa katika *Mtwara Corridor* na nani ametoa fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, suala la kuweka "X" sikulisahau kwa sababu maelekezo hayo ni ya *Regional Managers* wafanye. Ni fedha kiasi gani na ni nani amezitoa, kwa uhakika kabisa sasa hivi siwezi kumwambia, lakini fedha hizo zimepatikana kutoka *Kuwait Fund,* ndiyo waliotupa fedha hizo za kufanyia *feasibility study.* Baada ya kumaliza *feasibility study* zimebakia fedha sisi tukaamua kuzitumia fedha hizo zilizobakia kwenye mradi huo kufanya *design*. Nitakupatia takwimu sahihi wewe binafsi.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na taarifa ambayo iko kwenye *Internet* ni kwamba majirani zetu wa Msumbiji na Zambia wana-*support* ujenzi wa *Nakara Corridor* na *Beira Corridor* ambazo zikijengwa zitaua kabisa umuhimu wa *Mtwara Corridor.* Je, Serikali ina habari hizo na inafanya mikakati gani ili kutatua tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba, kuna *Nakara Corridor* na kuanzishwa kwa *Nakara Corridor* mimi nilikuwa shahidi, nilikuwepo Nakara. Serikali inafahamu kuna *Beira Corridor, Angola Corridor, Maputo Corridor* na *Central Corridor* na hizo zote ni *Geographical Economy* na sisi tunapanga hii na katika Bajeti Mwenyezi Mungu akijalia uhai mkiwepo, mtaona jinsi tunavyojitahidi kuutumia uchumi wa *Geography* kwenda huko huko ambapo wenzetu wanataka kuutoa. Kwa hiyo, tuvute subira. *(Makofi)*

Na. 15

**Mafuta ya Aina ya *JET A1***

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa gharama za uzalishaji wa umeme kwa Mradi wa *IPTL* kwa *TANESCO* ziko katika maeneo matatu ikiwa ni gharama maalum *(Fixed Cost)* zinazolipwa na aidha umeme uliozalishwa na kutumika au haukuzalishwa wala haukutumika na kiasi halisi cha umeme uliotumika na gharama za mafuta *JET A1* (mafuta ya ndege) yanayotumika kuendesha mitambo ya uzalishaji umeme Ubungo:-

(a) Je, bei ya mafuta hayo *JET A1* katika Soko la Dunia *(Arabian Gulf)* tarehe 1 Januari, 2004 ilikuwa kiasi gani kwa tani kwa dola za Kimarekani na pia ni sawa na shilingi ngapi za Tanzania?

(b) Je, bei ya mafuta hayo kwa mchanganuo wa gharama, bima na usafirishaji *(Cost Insurance and Freight - CIF), Dar es Salaam)* ni kiasi gani kwa tani kwa Dola za Marekani na fedha za Tanzania kwa tarehe 1 Januari, 2004?

(c) Je, mitambo hiyo ya kuzalisha umeme inatumia kiasi gani cha mafuta hayo *JET A1* kwa siku na ni kampuni gani inayowauzia *TANESCO* mafuta hayo kwa Mkataba tangu 2001 hadi 2004?

**NAIBUWAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hebert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gharama kwa *TANESCO* kutoka kwenye Mradi wa *IPTL* ziko katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni la uwezo wa mitambo *(Capacity Charge),* ambayo hulipwa kila mwezi hata kama mtambo haukuzalisha umeme, gharama hii ni shilingi bilioni 3.0 kwa mwezi. Eneo la pili, ni la umeme uliotumika *(Energy Charge),* ambayo hulipwa kutokana na *unit* zinazonunuliwa na *TANESCO*. Kwa mfano, umeme wote utakaozalishwa kwa kuendesha mitambo kwa uwezo wake wote wa *100 MW*, kwa mwezi huigharimu *TANESCO* takriban shilingi bilioni 5.0 . Kwa hiyo basi, kiwango cha chini na cha juu kwa mwezi ni shilingi bilioni 3.0 na shilingi bilioni 8.0 sawia.

Mheshimiwa Spika, mitambo ya Ubungo iko minne lakini miwili ni ya aina moja *(GT -10)* na mingine miwili ya aina nyingine *(LM 6000)*. Matumizi ya mafuta kwa mitambo ya aina hizo yanatofautiana kwa sababu ufanisi wake ni tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tarehe 1 Januari, 2004 ilikuwa ni sikukuu ya mwaka mpya, soko la mafuta halikufanya kazi siku hiyo. Hata hivyo, tarehe 2 Januari,

2004 bei ya mafuta katika Soko la Dunia *(Arabian Gulf)* ilikuwa ni Dola za Marekani 291.0 kwa tani, sawasawa na shilingi za Tanzania 311,864.70 kwa tani.

Bei ya mafuta *Jet A1* yanayotumiwa kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme Ubungo kwa mchanganuo wa gharama, bima na usafirishaji ni kama ifuatavyo: Bei ya kununulia kwenye soko *(Free on Board - FOB), USD 300.10/MT,* usafirishaji Dola 30.00 kwa tani, *Fixed Cost*, Dola 40.00 kwa tani pamoja na *Insurance Premium, Import Cost* Dola 10.00 kwa tani. Jumla Dola 380.01 kwa tani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, kuna aina mbili za mitambo ya *gas turbine* kama ifuatavyo:-

Mitambo ya *gas turbine LM 6000* ambayo matumizi yake ni wastani wa lita 10,000 kila mmoja kwa saa inapoendeshwa katika uwezo wake wa juu kabisa na Mitambo ya *GT-10* inatumia wastani wa lita 6000 kila mmoja kwa saa inapoendeshwa katika uwezo wake wa juu kabisa.

Tangu mwaka 2001 hadi Novemba, 2003, *TANESCO* ilikuwa na Mkataba wa ununuzi wa mafuta ya *Jet A1* na Kampuni za *ADDAX Tanzania Limited* na *BP Tanzania Limited*. Kuanzia Novemba, 2003 hadi sasa, *TANESCO* ina Mkataba na Kampuni ya *GAPCO Tanzania Limited.*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza:-

La kwanza, kwa kuwa gharama za kuendesha mitambo ya umeme pale Ubungo ni za juu kwa kutumia mafuta haya ya *Jet A1*, je, ni lini *Gas* ya Songo Songo kikamilifu itaanza kutumika pale ili kupunguza gharama hizi?

La Pili, kwa kuwa viwango vya faida katika bei za mafuta yanayoagizwa na Makampuni sasa hivi hazina udhibiti wowote wala hakuna chombo chochote kinachosimamia. Je, Serikali haioni kwamba, kwa sababu hiyo upo uwezekano mkubwa wa faida hizi kuwa kubwa na kusababisha bei za mafuta katika nchi kuwa kubwa sana? *(Makofi)*

**NAIBUWAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, gharama za kuendeshea mitambo ya *IPTL* kwa mafuta ya sasa ni kubwa sana, ndiyo maana Serikali ina mpango mahususi wa kubadilisha matumizi ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo ya *IPTL* kwa kutumia *gas* ya Songo Songo. Tayari Serikali imeshafanya majadiliano na Benki ya Dunia na kupata fedha za kuweza kubadilisha matumizi badala ya kutumia mafuta na kutumia *gas* na mpango huu mzima unategemewa kugharimu Dola za Marekani milioni 14 na katika utaratibu wake tayari kampuni ya *WASIRA* iliyouza mitambo ile, imeshapewa kazi ya kufanya *design* ili kufanya marekebisho ya mitambo ile na marekebisho haya yanakubalika ndani ya Mkataba wa ununuzi wa umeme wa *IPTL*.

Katika utaratibu uliopo tunatarajia kwamba, ifikapo Februari, 2005 *design* hiyo itakuwa imekamilika na ifikapo Desemba, 2005 mitambo hii itakuwa tayari imesharekebishwa na kuweza kuzalisha umeme kwa kutumia *gas.* Uzalishaji huu kwa kutumia gesi utaleta unafuu mkubwa katika bei ya umeme ambayo sasa hivi ni karibu senti sita na robo kwa *unit* hadi kufikia senti tatu na robo kwa *unit,* itapunguza sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chombo kinachosimamia mafuta, Wizara ipo kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wa shughuli za mafuta hapa nchini kwa sasa hivi. Lakini kama tunavyofahamu, tayari kuna chombo ambacho Serikali imekiunda cha *EWURA* na chombo hiki kitakapoanza kufanya kazi, basi tutakuwa katika utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba, biashara hii ya mafuta inaendeshwa vizuri.

Lakini si hivyo tu, Bunge hili Tukufu lilishapitisha sheria ya ushindani halali wa biashara *(Fair Competition)* na kupitia chombo hiki na *Commission* hii ya Biashara, Serikali inaweza kuhakikisha kwamba, wafanyabiashara hawa hawaundi umoja wa kuwakandamiza walaji na pale inapotokea basi *Commission* hii ina nguvu za kisheria za kuweza kuingilia kati.

Na. 16

**Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imeingia katika mtandao wa mawasiliano zikiwemo simu za mkononi ambazo husambazwa na makampuni kadhaa nchini; na kwa kuwa makampuni hayo yamejenga minara kadha wa kadha katika maeneo mengi nchini kuwezesha mawasiliano hayo:-

(a) Je, kiufundi haiwezekani minara hiyo kushirikiana baina ya makampuni kuliko ilivyo sasa kila kampuni kujenga minara yake na hivyo “kuchafua” mandhari ya nchi?

(b) Je, Serikali inapata malipo kiasi gani kwa kila mnara mmoja?

(c) Je, kiufundi na kwa kifupi, nini huwa kinatokea tangu mtumiaji wa simu kupiga simu, minara hiyo kuwezesha /kusafirisha mawimbi hadi mpigiwa simu kupokea simu aliyopigiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kiufundi kampuni za simu za mikononi zinaweza kushirikiana minara katika kutoa huduma zao kwa wateja. Kuna makampuni ambayo

tayari yameanza kushirikiana minara. Kwa makampuni ambayo bado hayajaanza kufanya hivyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imekuwa ikihimiza mazungumzo baina ya makampuni hayo na kimsingi makampuni yote yameonyesha nia ya kufanya hivyo ili kupunguza gharama na pia kulinda mazingira.

(b) Mheshimiwa Spika, kodi za minara zilizokuwa zikitozwa na Manispaa za Miji au Serikali za Mitaa, kodi hizo zilitofautiana viwango toka shilingi milioni tatu mpaka shilingi milioni tatu na laki tano kwa mnara mmoja. Hata hivyo, kodi hizo zilifutwa na Bunge letu kwenye Kikao cha Bajeti cha mwaka 2003/2004. Sababu kubwa ya kufutwa kodi hizo ni kuziwezesha kampuni za simu kuongeza mitandao yao.

(c) Mheshimiwa Spika, kiufundi *Transmission Process* kati ya mpiga simu na mpigiwa simu ni kwamba, mpiga simu anapopiga simu huanzisha mawasiliano baina ya simu yake ya mkononi na mnara ulioko karibu naye, ambao huwa umeunganishwa na mitambo mingine ya kutambua njia ya kwenda kwa mpigiwa simu. Mitambo hii pia hufanya mahesabu ya malipo ambayo mteja hutakiwa kulipia. Ikiwa mpigaji na mpigiwa simu wako mbali kwa mfano, Zanzibar na Mbeya, mawasiliano yanayotumika kuwaunganisha wateja hao ni yale ya Kampuni ya *TTCL.*

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi ningependa kujua kwamba binadamu anaweza kuujua ulimwengu kutokana na mawasiliano, lakini ulimwengu ukitaka kumjua binadamu inabidi angalau awe na simu ya mkononi na kitu kinachofanya simu za mikononi kuwa na bei ya juu Tanzania ni *VAT*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa *VAT* kwenye simu za mkononi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, ingawa hilo swali ni la Wizara ya Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ingefurahi sana kuona *VAT* inaondolewa katika mawasiliano hayo ili bei za simu ziwe nafuu, lakini pia tukubaliane kwamba, maombi yote tunayoyaomba ya mambo yetu mbalimbali yanatokana na makusanyo ya kodi ikiwemo *VAT,* kwa hiyo, kupanga ni kuchagua.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wizara Mawasiliano na Uchukuzi imo katika jitihada zake za kupunguza bei za simu za mkononi, ndiyo maana imeamua kuanzisha *system* mpya katika Jiji la Dar es Salaam kwa kutumia *card* mpya ambazo zina nambari za siri. Sasa kama wameweza kuanzisha katika Jiji la Dar es Salaam, je, mpango huo lini utaanzishwa Zanzibar na vilevile hapa Dodoma ili kupunguza wizi wa gharama za simu ambazo tunawekewa katika bili zetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba, katika juhudi za kumsaidia mtumiaji wa simu na kupunguza bei, *TTCL* imepanga na imeanzisha Mradi wa *Prepaid Service* kwa Jiji la Dar

es Salaam, lakini ni lengo na nia ya Serikali kuona shughuli hizi zinasambaa si Zanzibar na Dodoma tu, lakini katika sehemu nyingine zote.

Na. 17

**Viwango vya Gharama za Maingiliano kwenye Mawasiliano**

**MHE. BERNARD K. MEMBE (k.n.y. MHE. RAYNALD A. MROPE)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa imedhihirika kwamba miundombinu ya mawasiliano hapa nchini ni suala la lazima na si la anasa; na kwa kuwa mageuzi ya mabadiliko hayo duniani yanaenda kwa kasi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka viwango vya gharama za maingiliano *(Interconnection Tariffs)* kitakachokubalika na kampuni zote zinazotoa huduma za simu za mkononi *(Cellular Phone Operators)* ikiwemo Kampuni ya Simu ya *TTCL*?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufikia muafaka haraka kuhusu kiwango hicho cha maingiliano *(Interconnection Tariff)* kwa kuwa ni moja ya kigezo kinachosababisha gharama kubwa ya mawasiliano ya simu za mkononi?

(c) Je, Serikali inawapa matumaini gani Watanzania kuhusu mwelekeo na maendeleo ya matumizi ya simu za mkononi hasa kutokana na bei kubwa wanazolipa kutokana na matumizi ya simu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano, ikishirikiana na Kampuni ya Kitaalam kutoka Uingereza iitwayo *ANALYSYS* imefanya utafiti kuhusu gharama halisi za uunganishaji wa simu kwenye mitandao yote ya simu za msingi na zile za mikononi hapa nchini. Zoezi hili limekusudia kuwepo kwa suluhisho la kudumu la uunganishaji wa mitandao na kurahisisha maamuzi juu ya kiwango kipi cha uunganishaji wa simu kitozwe baina ya makampuni yanayounganishwa na hatimaye kujua gharama halisi za wateja watakazotozwa kwa kutumia huduma za simu.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kitaalam ya kutafuta gharama halisi imekamilika. *ANALYSYS* tayari wamewasilisha ripoti yao na mapendekezo yao kwa Mamlaka ya Mawasiliano. Kwa kuwa Bodi ya Mamlaka hiyo imeteuliwa hivi karibu, itakapokaa kwa mara ya kwanza, itazingatia pamoja na mambo mengine, umuhimu wa kutoa maamuzi ya kiwango kitakachotumika baina ya makampuni yanayounganishwa na kwa

kuzingatia mapendekezo yatokanayo kwenye utafiti wa mfumo huo maalum wa kujua gharama halisi za muingiliano.

Mheshimiwa Spika, gharama za maingiliano ni moja tu ya gharama za simu za mkononi zinazotumika na makampuni katika kupanga bei. Gharama nyingine ni uanzishaji wa mwito, urushaji mwito na kodi za aina mbalimbali. Hivyo basi, mwelekeo wa bei utatokana na jinsi gharama hizi zinavyopanda na kushuka. Hata hivyo, ni matumaini ya Serikali kwamba, bei halisi hatimaye zitawekwa na soko lenyewe kwa ushindani baina ya makampuni.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, je, atakubaliana na mimi kwamba bei za simu kwa watumiaji wa Tanzania ni kubwa mno, kwa sababu viwango vya kadi au bei za simu zile zinatozwa kwa *unit* na siyo dakika; je, Wizara itakuwa tayari kuzungumza na makampuni hayo kwenda katika viwango vya Kimataifa vya ku-*charge* kadi za simu kwa kutumia dakika na siyo *units* ambazo zinakwisha haraka zaidi ukilinganisha na wenzetu wa nchi zingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa yapo makampuni ambayo yanatoza simu kwa sekunde, lakini naomba niuchukue ushauri wake kwa kushirikiana na wenzetu kuona ni namna gani tunaweza kulifanyia kazi ipasavyo suala hili.

Na. 18

***CRDB* Kufungua Matawi yake Unguja na Pemba**

**MHE. MCHANDE SALIM MCHANDE** aliuliza:-

Kwa kuwa Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijin*i (CRDB)* ni benki ambayo inatoa mikopo kwa wakulima vijijini kwa upande wa Tanzania Bara; na kwa kuwa Serikali imekusudia kuifanya ardhi kuwa ndio kichocheo cha maendeleo hasa kwa wananchi wa vijijini ili kupunguza umaskini katika nchi yetu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua matawi yake Unguja na Pemba ili wananchi wa Tanzania Zanzibar wafaidike na huduma za benki hiyo badala ya kubaki kutoa huduma zake Tanzania Bara tu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mikopo wakulima wa Karafuu kupitia Benki hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mbunge wa Konde, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, iliyokuwa Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini au *Cooperative and Rural Development Bank,* ambayo ilikuwa Shirika la Umma, ilibinafsishwa na kuundwa upya kuwa Benki ya Biashara mwaka 1996 na kupewa jina jipya la *CRDB Bank Limited .* Hivyo Benki ya *CRDB* ya sasa ni benki binafsi, inaendesha shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kufungua matawi ya Benki hiyo huko Unguja na Pemba, kwa kuwa uamuzi wa kufanya hivyo ni wa benki yenyewe. Hata hivyo, Wizara yangu inayo habari kwamba, Benki ya *CRDB* tayari inafanya upembuzi yakinifu ili kubaini kama ufunguzi wa tawi Unguja na Pemba utakuwa wa faida au vinginevyo. Utafiti huo haujakamilika, lakini ni matarajio yetu kwamba, kama vigezo vitakuwa vizuri basi Benki hii itafungua tawi hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na sera tulizojiwekea, Serikali haina nia ya kuingilia biashara ya mabenki wala chombo kingine chochote. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuishawishi sio kuagiza Benki ya *CRDB* na taasisi nyingine za fedha nchini kutengeneza mikakati ya kutoa mikopo kwa wakulima, pamoja na kufanya tathmini ya uwezekano wa kuanzisha chombo pekee kwa kazi hii.

Na. 19

**Uzalishaji wa Tumbaku Mpanda**

**MHE. LEPHY B. GEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa takwimu chache za Zao la Tumbaku zilizoambatanishwa na swali hili zinaonyesha dhahiri kuwa wakulima wa tumbaku ni wazalishaji wa zao hilo kwa faida ya Kampuni ya Tumbaku na asilimia ya pato la mkulima sio hoja katika hali hiyo na kwa kuwa makampuni ya tumbaku yanajinufaisha sana na biashara ya pembejeo na tumbaku kwa pamoja. Je, kwa nini wakulima wa tumbaku Wilayani Mpanda wasijinasue na makucha hayo kupitia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa na Chama Kikuu cha Ushirika Wilayani Mpanda wapewe nafasi hiyo ya kuagiza pembejeo za wakulima walio ndani ya Vyama vya Ushirika kwa mazao yote?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lephy Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kilimo cha tumbaku kina mahitaji makubwa sana ya pembejeo, hususan mbolea. Kutokana na masharti magumu ya mikopo kwa wakulima wadogo wadogo ukiwepo ukosefu wa dhamana, kumesababisha wakulima wa tumbaku kupitia Vyama vyao vya Ushirika au vikundi, kushindwa kupata mikopo ya pembejeo au fedha kwa ajili ya kununulia pembejeo kutoka kwenye benki au taasisi zingine za fedha. Kwa hiyo, wakulima hao wamelazimika kutegemea mikopo ya pembejeo kutoka makampuni yanayonunua tumbaku kwa utaratibu unaompa fursa mnunuzi kumpatia mkulima kiasi cha pembejeo zinazohitajika kwa mkataba unaomtaka mzalishaji kumuuzia mnunuzi aliyempatia pembejeo tumbaku yote atakayozalisha ambapo deni lote la pembejeo hulipwa kutokana na thamani ya tumbaku iliyouzwa.

Baada ya maelezo hayo mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lephy Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za mauzo ya tumbaku iliyozalishwa katika misimu ya 1998/1999 hadi 2002/2003 madeni yote ya pembejeo katika Wilaya ya Mpanda yalichukua wastani wa asilimia 46 ya thamani ya mauzo ya tumbaku. Kiasi cha fedha walicholipwa wakulima kupitia katika Vyama vyao vya Msingi kilikuwa ni asilimia 54 ya mauzo. Uwiano huu hafifu wa thamani ya madeni na malipo kwa wakulima ulitokana na sababu zifuatazo:-

(i) Tija ya uzalishaji wa tumbaku kwa hekta katika Wilaya ya Mpanda ilikuwa takriban kilo 870 ikilinganishwa na uwezo uliopo wa kuzalisha kilo 1,500 kwa hekta moja. Tija hiyo ya kiwango cha chini wakati gharama za pembejeo kwa hekta moja ya tumbaku zinabaki zile zile ambazo ni shilingi 532,000/= inampunguzia sana kipato mkulima wa tumbaku;

(ii) Kiwango cha chini cha ubora wa tumbaku iliyozalishwa katika misimu ya kilimo ya 1998/1999 hadi 2001/2002, kilisababisha bei ya mkulima kuwa ndogo, ambapo kwa wastani mkulima alilipwa Sh. 525/= kwa kilo; na

(iii) Baadhi ya wakulima wasio waaminifu katika Vyama vya Ushirika vya Msingi ambavyo viliingia Mikataba na wanunuzi wa tumbaku kwa niaba ya wakulima, walichukua pembejeo za tumbaku kisha wakaziuza kwa wakulima wa mazao mengine badala ya kuzalisha tumbaku kama walivyokuwa wamekubaliana. Hali hii huathiri sana mapato ya mkulima kwa sababu deni la pembejeo zote hukatwa kwenye mauzo ya tumbaku ya vyama husika kwa asilimia mia moja wakati pembejeo hizo hazikuzalisha tumbaku kama ilivyokuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni vema wakulima wa tumbaku Wilayani Mpanda na kwingineko, kupata mikopo ya pembejeo bila kuhusisha wanunuzi wa tumbaku ili kujiweka katika nafasi bora zaidi katika biashara ya tumbaku. Kutokana na ukweli kwamba, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa hauwezi peke yake kukidhi mahitaji ya mikopo kwa zao la tumbaku na mazao mengine, wakulima wanahimizwa kuanzisha kwa nguvu zao wenyewe, mifuko ya kuendeleza mazao, ikiwemo huduma ya pembejeo. Aidha, wakulima wanahimizwa kuanzisha Vyama vya

Kuweka na Kukopa *(SACCOS),* ambavyo watajiwekeaakiba na baadaye kukopeshana ili kukidhi mahitaji ya pembejeo. Mfuko wa Pembejeo wa Taifa umekuwa ukiongezea nguvu ya ukopeshaji katika mifuko hiyo kwa kutoa mikopo nafuu.

Aidha, Serikali inaimarisha elimu ya ushirika na matumizi ya sheria katika Vyama vya Ushirika ili visimamie na kudhibiti vilivyo mikataba, matumizi na marejesho ya mikopo ya pembejeo na kuondoa matatizo yatokanayo na ubadhirifu. Mikakati zaidi ya kushughulikia suala la upatikanaji wa uhakika wa pembejeo kwa wakulima nchini itatolewa na Serikali kupitia kwa Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na Kilimo na Chakula katika hotuba zao za Bajeti katika Bunge hili linaloendelea hivi sasa. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ninataka kufahamu je, Bodi ya Tumbaku itamsaidiaje mkulima wa tumbaku wa Wilaya ya Mpanda ili aweze kunufaika na punguzo la bei ya pembejeo iliyotolewa kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wakati tayari mikataba na makampuni ya tumbaku ilishafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimetoa maelezo katika jibu langu la msingi hapa kwamba, maelezo ya kina na mikakati zaidi yatatolewa wakati wa hotuba za bajeti za Mawaziri wahusika. Lakini kimahususi kufuatana na swali lake kwamba wanunuzi hawa binafsi wameshaingia mikataba na wakulima na kwa hiyo wangependa wapate ile nafuu ya ruzuku ya pembejeo ambayo walipewa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Nataka tu nieleze kwamba, ile nafuu ilitolewa kwa ajili ya mazao ya nafaka ambayo ni ya chakula na kama mnavyofahamu kwamba, nafuu ile ilitolewa kwa ajili ya Mikoa ile ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni *the big four* na u- *big four* huo umetokana na uzalishaji wa chakula. Kwa hiyo, hiyo haihusiki na zao la tumbaku kama anavyoomba Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wakulima wengi wameshagundua tatizo hilo la kujiingiza katika mikataba na makampuni ambayo mara zote yamekuwa yakiwaweka katika hali mbaya ya uzalishaji na kwa kuwa wengi sasa wameshaanzisha Vyama vya Ushirika na *SACCOS* ili kuweza kujiimarisha zaidi. Je, Wizara haioni kwamba sasa umefika wakati muafaka wa kuvisaidia Vyama hivyo kuwa na nguvu ili kuviwezesha kuwahudumia wakulima pembejeo na mambo mengine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa jitihada zake katika kuhamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo. Sisi tunaungana naye na jitihada zake hizo. Lakini sasa kama alivyouliza kwamba Serikali itavisaidiaje vyama hivi, kusema kweli kazi ya Serikali sasa hivi ndiyo hiyo ya kuhamasisha vyama hivi vianzishwe kwa wingi na viimarike. Hivi sasa programu tulizonazo ni pamoja na

kuanzisha au kuikamilisha programu yetu ya *Co-operative Reforms,* ambayo itazingatia utekelezaji wa sheria mpya ya ushirika, ambapo vyote kwa pamoja vinalenga katika kuwaimarisha wanachama wa vyama vya ushirika waliokwishajiunga pamoja ili waweze kuendesha vyama vyao kwa ukamilifu. Kwa hiyo, Serikali iko pamoja na wananchi wote walioanzisha vyama vya ushirika pamoja na wale ambao wanakusudia kuanzisha. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba haya Makampuni makubwa ya tumbaku yaliamua kuungana ili yapate nguvu ya kuweza kuwanyonya wakulima na kwamba bei wanayowapa wakulima wetu sasa haizingatii gharama halisi ya uzalishaji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, suala la haya Makampuni binafsi au wanunuzi binafsi ambao sio waaminifu kuunda umoja usio rasmi na njia zingine zozote ambazo haziendani na ushindani usio wa haki, Serikali inafahamu na inajitahidi kupigana nao vita kwa kuzingatia kwamba sheria zilizopo zinafuatwa. Lakini Serikali inatoa wito kwamba, kwa kushirikiana na vyombo vingine, wakiwemo hata Waheshimiwa Wabunge, kutoa taarifa kwa wale wote ambao wanakiuka sheria hizi ili tuweze kushirikiana katika kukabiliana na vitendo hivyo viovu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na sasa kuna matangazo ya vikao vya Kamati kwa siku ya leo. Kamati tatu zimepangiwa kukutana. Ya kwanza ni Kamati ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Omar Kwaang'w, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Huduma za Jamii wakutane leo tarehe 9 Juni, 2004 chumba Na. 133 saa 5.00 asubuhi.

Kamati ya pili, ni Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC),* Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anawaomba Wajumbe wa *PAC* wakutane saa 5.00 asubuhi hiyo hiyo Ukumbi Na. 219. Kamati ya tatu, ni Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wakutane leo mara baada ya kipindi hiki cha maswali kwenye Ukumbi Na. 231. Mwisho wa matangazo.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria za Uchaguzi wa Mwaka 2004 *(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria unaoitwa *The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2004* usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa sheria zifuatazo: Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya mwaka 1979.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, pamoja na Kamati yake ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuuchambua kwa kina Muswada huu na hivyo kuiwezesha Serikali kuuboresha zaidi na sasa kuwasilishwa Bungeni. Marekebisho makubwa yanayopendekezwa kufanywa katika sheria hizi zote mbili yanakusudia kuweka utaratibu wa masharti ya kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linalobainishwa katika ibara ya 5(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977. Inasema: "Bunge litatunga Sheria ya Uchaguzi na kuweka masharti kuhusu kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kuweka utaratibu wa kurekebisha yaliyomo katika Daftari hilo."

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yaliyofanywa pamoja na kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inatoa fursa ya kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, sheria zilizopo za Uchaguzi haziiwezeshi Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuanzisha kikamilifu Daftari la Wapiga Kura la nchi nzima na kuandikisha Wapiga Kura katika Daftari hilo kwani mfumo wa sasa unatoa mamlaka ya kuandikisha wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo ya uchaguzi na kumbukumbu zote huishia katika majimbo hayo husika. Aidha, kumbukumbu hizo hutakiwa kuharibiwa baada ya miezi sita tokea matokeo ya Uchaguzi yatakapotangazwa. Hali hii haiiwezeshi Tume kuwa na kumbukumbu za Wapiga Kura wa nchi nzima. Hivyo, marekebisho ya sheria yataiwezesha Tume kuwa na kumbukumbu za Wapiga Kura, zitakazojumuishwa kwa pamoja kwa ajili ya kuandaa Daftari la Wapiga Kura. Aidha, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya mwaka 1979, haikuwa imerekebishwa kabisa kuruhusu uanzishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanayofanywa katika sheria zote mbili yanakusudia kuanzisha Tume ya Taifa, kuendesha na kusimamia Uchaguzi kwa ufanisi zaidi hasa ukizingatia uzoefu uliopatikana katika Uchaguzi mwaka 2000 ambao bado haujaweza kuathiri Uchaguzi wa mwaka 1985 na siku zijazo. Aidha, marekebisho haya yataipa Tume Mamlaka na fursa ya kusahihisha makosa ambayo hayakustahili yaliyojitokeza katika Uchaguzi ndani ya kipindi cha Uchaguzi badala ya kusubiri matokeo ya Uchaguzi kumalizika na malalamiko kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, sheria ya kwanza kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985 ambapo kifungu cha 2 cha sheria hiyo kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kufafanua misamiati mipya ambayo inatumika katika sheria hiyo kwa ajili ya kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura . Kwa mujibu wa sheria hiyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, haina uwezo kutoa wala kuratibu vyombo vinavyotoa elimu kwa mpiga kura. Hivyo basi, inapendekezwa kuongezwa kifungu kipya cha 4(c) ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutekeleza jukumu la kusimamia kwa karibu elimu ya Wapiga Kura itakayotolewa na watu wa vyombo vinavyotoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuongezwa kifungu kipya cha 7(a) ili kuwafanya Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji, Jiji, Manispaa na Wilaya, kuwa na Maafisa Waandikishaji wa Wapiga Kura katika Majimbo ya Uchaguzi. Hii itaiwezesha Tume kuwatumia Watendaji hao katika uandikishaji Wapiga Kura kwenye Majimbo ya Uchaguzi na Kata. Marekebisho haya yataoanisha utaratibu uliopo kisheria wa Wakurugenzi wa Halmashauri hiyo au Wasimamizi wa Uchaguzi. Hata hivyo, endapo Tume haitabaini yenyewe na kutokana na kupokea malalamiko dhidi ya uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmashauri yoyote kwa Afisa Waandikishaji itamteua mtumishi wa umma na mwingine badala ya Wakurugenzi wa Halmashauri husika kuwa Afisa Uandikishaji wa Halmashauri inayokusudia. Vile vile marekebisho hayo yatawezesha Tume kuteua Maafisa Waandikishaji Wasaidizi kutoka miongoni mwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10 kinaelekeza kuwa mtu atakuwa na sifa ya kuandikishwa endapo ana umri wa miaka 18. Kwa kuwa uandikishaji wa Wapiga Kura utaanza kufanyika mwaka mmoja tu kabla ya Uchaguzi, kutokana na ufinyu wa muda kwa ajili ya kuandikisha Daftari hilo, hakutakuwa na fursa ya kufanya uboreshaji na kuandikisha tena Wapiga Kura watakaokuwa na miaka 18 ifikapo mwaka 2005. Hivyo basi, kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha wale ambao hawajatimiza umri wa miaka 18 wakati wa uandikishaji lakini watakuwa wametimiza miaka 18 siku ya kupiga kura, kuweza kuandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Uandikishwaji utafanyika mwaka huu. Aidha, watu wa aina hii watatakiwa kuthibitisha umri wao ili waweze kuandikishwa kama Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, uandaaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni mchakato mrefu. Tume baada ya kuandikisha Wapiga Kura kwa mara ya kwanza, itapaswa kuingiza na kuchambua taarifa ya Wapiga Kura katika *Central Voter Database* na katika daftari la awali la wapiga kura yaani *Provision Voters Register. Provision Voters Register* itatumika kama rasimu kwenye Daftari kwa madhumuni yafuatayo: Kwanza, kuweka mahali pawazi ili mtu yeyote aweze kukagua usahihi wa jina lake au uhalali wa watakaokuwemo katika Daftari hilo. Pili, kutambua watu wasiostahili kuwemo katika Daftari la awali ili wawekewe pingamizi. Tatu, kuona usahihi wa majina au taarifa za wapiga kura na nne, kuona makosa yanayoweza kujitokeza na kufanya marekebisho yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 12, Wasimamizi wa Uchaguzi ndio watakaopewa jukumu la kutunza Daftari la Wapiga Kura katika majimbo yao. Mkurugenzi wa Uchaguzi hana mamlaka hayo kwa kuwa sasa litaandaliwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 12. Hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa na mamlaka au wajibu wa kutunza na kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Vile vile Tume inaomba kutoa maelekezo kwa Watendaji wanaohusika na kuandikisha wapiga kura. Aidha, Watendaji hao watawasilisha taarifa za wapiga kura izijumuishe kwa pamoja na kuingiza katika kompyuta kwa njia ya *scanning* na hatimaye kutangaza Daftari la Wapiga Kura la nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 12(a) na kuongeza kifungu kidogo cha 2, kuanzisha Tume kuwa na mamlaka ya uandikishaji wa wapiga kura waliopo Tanzania Zanzibar, tunastahili kupiga kura katika Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Kwa sheria iliyopo, Wapiga Kura hao hawawezi kuandikishwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar na vile vile hawastahili kupiga kura katika Uchaguzi Zanzibar. Aidha, Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina Mamlaka ya kuandikisha.

Mheshimiwa Spika, eneo linalohusu muda wa kuandikisha wapiga kura nalo lilipendekezwa kurekebishwa. Mfumo uliopo huu wa sheria, unahitaji wapiga kura kuandikishwa ndani ya miezi sita kabla ya tarehe ya Uchaguzi. Ni dhahiri kwamba, muda huo hautoshi kuanzisha Daftari la Kupiga Kura kwani teknolojia inayotumika inahitaji si chini ya miezi 10 kutekeleza hatua zote za kulikamilisha Daftari hilo tayari kwa ajili ya Uchaguzi wa mwaka 2005. Ili kukidhi muda wa kuanzisha Daftari la Kupiga Kura, inapendekezwa kuwa kifungu cha 15 kirekebishwe Tume iweze kupanga muda wa uandikishaji Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21 kinafanyiwa marekebisho ya rufaa zote dhidi ya uandikishaji wa wapiga kura zishughulikiwe katika Mahakama za Wilaya badala ya Mahakama za Mahakimu Wakazi. Vile vile inapendekezwa kuwa muda wa kushughulikia rufaa upunguzwe kutoka siku 21 na kuwa siku 14 toka rufaa ilipopelekwa Mahakamani. Marekebisho hayo yanakusudia kurahisisha ukataji wa uwasilishaji wa rufaa kwa sababu Mahakama za Wilaya ni nyingi kuliko Mahakama za Mahakimu Wakazi na zipo karibu zaidi na wananchi walio wengi. Hii itasaidia rufaa dhidi ya uanzishaji uwasilisho na kusikilizwa mapema na kwa haraka zaidi. Hali hii ni muhimu sana kwa ufanisi wa Daftari kwani marekebisho yatakapopatikana, maamuzi ya Mahakama yatafanywa mapema.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpisha Afisa Mwandikishaji, kulazimika kisheria kuweka mahali pa wazi Daftari la Awali ili Wapiga Kura walikague kuangalia usahihi wa majina yao na pia kujiridhisha kama waliomo walistahili kuwa Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 26 hadi 27 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili muda wa kushughulikia pingamizi na rufaa dhidi ya uandikishaji upunguzwe kutoka siku 14 hadi siku 7 toka pingamizi lilipowasilishwa. Vile vile inapendekezwa kuwa muda wa siku za rufaa dhidi ya uanzishaji upunguzwe siku 20 hadi 24 toka rufaa ilipowasilishwa Mahakamani. Hali hii itawezesha pingamizi za rufaa kushughulikiwa mapema ili kuiwezeshwa Tume kufanya marekebisho yaliyohitajika kulikamilisha Daftari la Awali kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa inampa mamlaka Msimamizi wa Uchaguzi, kurekebisha taarifa ya wapiga kura baada ya maamuzi ya Mahakama kufuta rufaa dhidi ya uanzishaji. Kwa kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ndiye atatunza Daftari la Kupiga Kura, inapendekezwa kuwa kifungu cha 28 kifanyiwe marekebisho ili Mkurugenzi wa Uchaguzi aweze kuletewa na Maafisa Waandikishaji, maamuzi ya Mahakama kuhusu

rufaa ya uanzishwaji. Utaratibu huu utawezesha Tume kusahihisha na kuwa na kumbukumbu sahihi za wapiga kura na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Kifungu cha 38 kinapendekezwa kurekebishwa ili Wagombea Urais na Makamu wa Rais, waweze kisheria kula kiapo cha kuwa na sifa za kuwa Wagombea Urais mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa. Hapo awali sheria ilikuwa inahitaji mgombea Urais au Makamu wa Rais, kula kiapo mbele ya Hakimu.

Vifungu vya 68(a) na 81 vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kubainisha zaidi dhana ya kura halali ambazo mgombea atapata katika Uchaguzi. Kifungu cha 46 nacho kinaelekeza kuwa endapo Uchaguzi utashindwa kufanyika na utashindwa kuendelea kufanyika siku hiyo, Tume ipange siku nyingine ya Uchaguzi baada ya siku 60 au 90. Hali hii inaweza kuathiri na kuchelewesha kutangazwa kwa matokeo ya Uchaguzi wa Rais kwa sababu matokeo hayo hayawezi kutangazwa kabla ya Uchaguzi wa Rais na kukamilika katika majimbo yote na kura kuhesabiwa. Kwa hali hiyo inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 46 ili Tume iwe na mamlaka ya kupanga tarehe nyingine ya Uchaguzi utakaoshindwa kufanyika au utakaoshindwa kuendelea kufanyika siku hiyo ya kupiga kura katika muda ambao Tume itaona inafaa badala ya kulalamika kusubiri siku 60 au 90.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa, Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba, hali ya Wagombea kujitoa katika Uchaguzi, husababisha usumbufu, gharama na athari katika Uchaguzi. Hali hiyo ilikuwa ikijionyesha katika chaguzi mbalimbali. Kwa sasa mgombea anatarajiwa kujitoa katika Uchaguzi kwa kuandika barua kwa ajili hiyo kwa Msimamizi wa Uchaguzi. Uzoefu umeonyesha kuwa, utaratibu huu hautoshelezi kuthibitisha mgombea kujitoa, kwa mantiki hiyo, inapendekezwa kuwa kifungu cha 48 kifanyiwe marekebisho ili kiweke sharti kwamba, mgombea anajitoa katika Uchaguzi kwa kula kiapo kwa ajili hiyo mbele ya Hakimu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 51 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili Msimamizi wa Uchaguzi wakati wa kampeni za Uchaguzi alazimike kuitisha Mkutano wa Wagombea, mawakala wa vyama vyao ili kuratibu ratiba ya mkutano wa kampeni ya uchaguzi. Marekebisho haya yataepusha uwezekano wa mikutano ya Wagombea wa vyama tofauti vya siasa na kugongana. Pia itahakikisha wazi uwasilishaji wa Wagombea wa vyama vyao vya siasa katika kuandaa ratiba ya mikutano ya Kampeni.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mwaka 2000 kifungu cha 59 kilifanyiwa marekebisho ili kuainisha mambo yanayotakiwa kuwemo katika karatasi ya kupiga kura. Marekebisho hayo hayakufanyika katika kifungu cha 56. Hivyo, kifungu cha 56 kinafanyiwa marekebisho ili nacho kiainishe mambo hayo. Marekebisho hayo pia yataiwezesha Tume kuandaa mfano wa karatasi ya kura, utakaokuwa na jina, picha na anwani za Wagombea na nembo za vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 67 kinafanyiwa marekebisho ili kama upigaji kura umeanza katika kituo na kushindwa kuendelea kufanyika kutokana na vurugu, uweze kuahirishwa na Msimamizi wa Kituo cha kupigia kura mpaka siku ya pili, hii ni

kama tu kuna wapiga kura katika Daftari ambao hawajapiga kura. Utaratibu huu utaondoa uwezekano usio na sababu ya wapigaji kura kuahirishwa hadi siku nyingine wakati wapiga kura wote watakuwa tayari wameshapiga kura.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 74 kinafanyiwa marekebisho ili mgombea aliyejitoa katika Uchaguzi baada ya karatasi ya kura kuchapishwa, anapigiwa kura, kura hizi zichukuliwe kuwa zimeharibika. Kwa kuongeza kifungu kipya cha 90(a) ili kuwawajibisha Watendaji watakaovuruga kwa makusudi taratibu za uanzishaji wa Daftari la Wapiga Kura. Aidha, kifungu hiki kipya kinachopendekezwa kinaoana na dhana ya kuwepo kwa Maafisa Waandikishaji wa kupiga kura waliopendekezwa katika Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 104 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kisomeke kuwa siku ya Uchaguzi mtu yeyote hataruhusiwa kuvaa sare, kadi au picha inayoashiria kumwunga mkono mgombea yeyote katika maeneo karibu na vituo vya kupigia kura, hali hii huzuia kampeni ya siku ya kupiga kura. Kifungu cha 107 na 114 inapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa kifungu (c) ili kumwezesha Mkurugenzi wa Uchaguzi kubaki na mamlaka ya kumwondoa katika Daftari mtu yeyote ambaye anapatikana na hatia kwa makosa ya rushwa katika Uchaguzi. Awali kwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi ndiyo alikuwa anaandaa orodha ya wapiga kura, yeye ndiyo alikuwa na fursa ya kufanya marekebisho ya kumwondoa mhusika baada ya kuarifiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi kuhusu uamuzi wa Mahakama. Kutokana na kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Mkurugenzi wa Uchaguzi ndiye anayetunza *Central Voter Database* na ndiyo atakayeweza kufanya marekebisho yanayohusika. Kifungu cha 116 kinapendekezwa kifanyiwe marekebisho ili kuondoa dhana ya kura bubu iliyokwisha kuondolewa katika sheria hiyo tangu mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, sheria ya pili inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Serikali ya Mitaa ya mwaka 1979. Marekebisho yanayopendekezwa kufanywa katika sheria hii, ni kwamba, sheria inakusudia kuoanisha marekebisho yanayofanyika ya kuisaidia Sheria ya Uchaguzi Namba 1 ya mwaka 1985 ili kuleta uwiano katika taratibu za kuandikisha Wapiga Kura kaitika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Uchaguzi wa Madiwani. Kama ilivyoelezwa hapo nyuma, sheria hii kama ilivyo hivi sasa, haitoi kabisa mamlaka kwa Tume kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Madiwani. Aidha, yako maeneo mengine ambayo mapendekezo ya marekebisho yake yanafanana na marekebisho yatapendekezwa katika Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985. Kwa hiyo, hayana maelezo tofauti.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yaliyoainishwa hapa chini yanalenga katika kuondoa kasoro na mapungufu yaliyojitokeza katika Uchaguzi wa mwaka 2000 na hivyo kuanzisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendesha Uchaguzi wa Madiwani kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 48 kinafanyiwa marekebisho ili muda uliopo kufanya Uchaguzi Mdogo wa Madiwani baada ya uteuzi wa Wagombea uwe siku 60 au 90 kama ilivyo kwa upande wa Uchaguzi Mdogo wa Wabunge. Marekebisho haya

yataiwezesha Tume ya Uchaguzi kufanya chaguzi ndogo katika muda mfupi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa ikizingatiwa kuwa eneo la Kata ni dogo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kupungua kwa muda wa kufanya Uchaguzi utapunguza gharama kubwa za Uchaguzi. Napenda kuelezea pia kwamba, tulipata nafasi ya *public hearing* na viongozi wa vyama vya siasa wote takriban Wenyeviti wao walikuwepo Dar es Salaam na kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kukushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niseme tu kwamba, karatasi ya marekebisho kwenye Muswada huu zimeshagawiwa kwa Wabunge, naomba basi wakati wa mjadala tuzingatie vile vile haya marekebisho ambayo yamefanyika.

Sasa namwita Mwakilishi wa Kamati iliyochambua Muswada huu, Mwenyekiti mwenyewe ni Mheshimiwa Athumani Janguo. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 70(2) Toleo la mwaka 2004 na kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa maoni ya Kamati hii kuhusu Muswada wa Sheria uitwao *The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2004.*

Kabla sijatoa maoni ya Kamati ni muhimu nifanye mambo mawili yafuatayo: Kwanza kwa niaba ya Kamati, napenda kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga na Chama cha Mapinduzi, kwa ushindi wao wa kishindo katika Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Bariadi Mashariki. *(Makofi)*

Pili, napenda kutoa salamu zangu za rambirambi kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, awape subira na aiweke roho yake mahali pema peponi. *(Amen)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambao walichambua Muswada huu na kuuboresha kama ifuatavyo: Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Makamu Mwenyekiti,

Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah S. Fundikira, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary H. K. Nyerere, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa George F. Mlawa, Mheshimiwa Paschal C. Degera na Mheshimiwa Nimrod E. Mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 69(1), Kamati ililetewa Muswada huu unaopendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbili zifuatazo: Sheria ya Uchaguzi Namba 1 ya mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Na. 4 ya mwaka 1979.

Mheshimiwa Spika, aidha, kama alivyoeleza mtoa mada, kimsingi marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hizi mbili yanalenga kuweka utaratibu wa masharti ya kuanzisha ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kuweka masharti yanayohusu uandikishaji wa Wapiga Kura na kuainisha majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na wote watakaohusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupokea Muswada huu rasmi, kwa mujibu wa kanuni, iliamua kupata maoni mengi kadri inavyowezekana kutoka kwa wadau mbalimbali hususan Viongozi wa Vyama vya Siasa vilivyosajiliwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kazi hii ya kupata maoni ya wadau ilifanyika Mjini Dar es Salaam tarehe 3 Juni, 2004. Kamati inawashukuru sana Viongozi hao wa Vyama vya Siasa kwa maoni ambayo yamesaidia katika kuuboresha Muswada huu.

Baada ya kupata maoni ya wadau muhimu katika kuboresha Muswada huu, Kamati ilikutana hapa Dodoma tarehe 7 Juni, 2004 kuuchambua Muswada. Katika kuuchambua Muswada huu, kimsingi Wajumbe wa Kamati wamekubaliana na mapendekezo ya marekebisho yaliyomo kwenye Muswada kwamba, pamoja na Katiba ya Nchi kutoa fursa ya kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Sheria za Uchaguzi zilizopo hivi sasa hazitoi nafasi nzuri kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuanzisha kikamilifu Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa umuhimu wa kuwepo kwa Daftari hili ni mkubwa kwa Taifa kwani hiyo ndiyo njia pekee ya kuwa na kumbukumbu za kudumu za Wapiga Kura. Isitoshe Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litaondoa malalamiko dhidi ya watu wasiostahili kupiga kura wasiweze tena kujiingiza katika upigaji kura. Katiba ya Nchi inatamka kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kuwa jambo ambalo linahitaji kuzifanyia marekebisho Sheria Na. 1 ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria Namba 4 ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1979. Aidha, upungufu mwingine uliopo hivi sasa ni kwamba, wakati Katiba ya Nchi inatamka kuanzishwa kwa Daftari la

Kudumu la Wapiga Kura Sheria ya Uchaguzi ya Madiwani Na. 4 ya mwaka 1979 haijafanyiwa marekebisho kuhusu uanzishaji wa Daftari hili la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, marekebisho ya sheria zote mbili yataoanisha taratibu za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani katika hatua zote zifuatazo: Moja uandikishaji wapiga kura, mbili uteuzi wa Wagombea na tatu upigaji kura wenyewe. Taratibu hizi hazikuwa zinafanana kwa hiyo Muswada huu unazingatia upungufu huo kwa lengo la kuboresha shughuli nzima ya Uchaguzi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza mambo haya ya ujumla, naomba sasa nielezee maoni ya Kamati kwa vifungu vilivyofanyiwa marekebisho.

Kwanza, Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985, kifungu cha 2 cha sheria kinafanyiwa marekebisho ili kufafanua misamiati mipya ambayo ni Daftari la Wapiga Kura, Afisa Mwandikishaji na kadi ya kupigia kura. Kimeongezwa kifungu kipya cha 4(c) kinachoipa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jukumu la kutoa elimu ya Wapiga Kura nchi nzima na kuratibu vyombo vitakavyotoa elimu hiyo. Awali Tume haikuwa na uwezo wa kutoa au kuratibu utoaji wa elimu hiyo. Marekebisho haya yataipa Tume ya Uchaguzi nguvu ya kisheria ya kuelimisha Wapiga Kura ili waweze kuitumia vizuri haki yao ya kimsingi katika Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kimeongezwa kifungu cha 7(a) ili kuwafanya Wakurugenzi wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya wawe Maafisa Waandikishaji kura katika Majimbo ya Uchaguzi. Aidha, Tume ya Uchaguzi itakuwa na uwezo wa kisheria wa kuteua Maafisa Waandikishaji Wasaidizi miongoni mwa watumishi wengine wa umma. Pendekezo hili lilipingwa vikali sana na wadau lakini Kamati, baada ya kutafakari umuhimu wa kuwa na waandikishaji watakaoweza kuwajibishwa endapo watavuruga uandikishwaji, Kamati imeona ikubaliane na pendekezo la Serikali.

Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kuwawezesha wale ambao hawajatimiza umri wa miaka 18 wakati wa uandikishaji lakini watakuwa wametimiza miaka 18 siku ya kupiga kura waweze kuandikishwa katika Daftari la Wapiga Kura. Kamati haina kipingamizi na pendekezo hili.

Mheshimiwa Spika, kifungu kingine kinachoongezwa ni cha 11(A), ambacho kina shabaha ya kuondoa wasi wasi miongoni mwa wadau wa Uchaguzi nchini ili kufanikisha azma hiyo ya Daftari la Awali la Wapiga Kura. Kwanza, litawekwa mahali pa wazi ili mtu yeyote aweze kukagua usahihi wa jina lake na uhalali wa wengine walioandikishwa. Pili, kutambua watu wasiostahili ili kuwawekea pingamizi. Tatu, kuona makosa yoyote mengine ili yasahihishwe. Kamati yangu inaiafiki nyongeza hii.

Marekebisho mengine yanayopendekezwa ni katika kifungu cha 12 ili kuipa Mamlaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutunza na kuboresha Daftari la Wapiga Kura. Aidha, Muswada unapendekeza kuongeza kifungu cha 12(a) ili kuiwezesha Tume kuwa na mamlaka ya kuandikisha Wapiga Kura walio Tanzania Visiwani ambao wanastahili kupiga kura katika Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kamati inakubaliana na

rekebisho hili kwani litaondoa usumbufu wa kuandikishwa mara mbili kwa Wapiga Kura wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unapendekeza marekebisho ya kifungu Na. 15 ili kuipa Tume mamlaka ya kupanga muda na uboreshaji wa Daftari la Kupiga Kura. Marekebisho yanayopendekezwa katika vifungu vya 17, 18 na 19 yanaipa Tume ya Kudumu ya Uchaguzi mamlaka ya kutoa maamuzi yatakayosaidia kulisimamia vizuri sana Daftari la Uchaguzi. Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na pendekezo la kurekebisha kifungu namba 21 ili rufaa zote dhidi ya uandikishaji wa Wapiga Kura zishughulikiwe katika Mahakama za Wilaya badala ya Mahakama za Mahakimu Wakazi. Pia Kamati inaafiki punguzo la muda wa kushughulikia rufaa kutoka siku 21 hadi siku 14 tokea rufaa inapopelekwa Mahakamani.

Vile vile Kamati inaafiki marekebisho katika vifungu vya 26 na 27 yanayopunguza muda wa kushughulikia pingamizi na rufaa dhidi ya uandikishaji kutoka siku 21 hadi 14. Kamati inakubaliana na rekebisho katika kifungu cha 28 kwa kuwa litaiwezesha Tume kuwa na kumbukumbu sahihi za Wapiga Kura katika Daftari la Wapiga Kura.

Marekebisho yanayokusudiwa katika vifungu vya 38(a) na 81 yenye nia ya kuwafanya Wagombea Urais kubainisha zaidi dhana ya kura halali za mgombea, Kamati inayaafiki. Kamati inakubaliana na pendekezo la kurekebisha kifungu Na. 46 linayoipa Tume Mamlaka ya kupanga tarehe nyingine itakayoona inafaa badala ya kulazimisha kusubiri siku 60 hadi 90 pale unaposhindikana kuendelea.

Rekebisho katika kifungu cha 38 Kamati inaliafiki kwani litaondoa mizozo pale mgombea anapojitoa na akaapa mbele ya Hakimu. Wakati huo huo rekebisho katika kifungu cha 51 Kamati inaliafiki kwa kuwa litaondoa migongano ya vyama mbalimbali vya siasa nyakati za kampeni.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 27 kinafanyiwa marekebisho ili kama upigaji kura umeanza katika kituo na ukashindwa kuendelea kufanyika kutokana na vurugu, kiahirishwe na msimamizi wa kituo cha kupiga kura mpaka siku ya pili kama tu kuna wapiga kura katika daftari ambao watakuwa hawajapiga kura, kwani Kamati haioni mantiki ya utaratibu wa sasa wa kuahirisha upigaji kura hadi siku nyingine wakati wapigakura wote watakuwa tayari wameshapiga kura.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 74 kinafanyiwa marekebisho ili mgombea aliyejitoa katika uchaguzi baada ya karatasi za kura kuchapishwa na akapigiwa kura, kura hizo zichukuliwe kuwa zimeharibika. Kamati inakubaliana na utaratibu huu unaopendekezwa kwani utaepusha uwezekano wa mtu ambaye ameshajitoa katika uchaguzi kupigiwa kura na akachaguliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dhana ya kura bubu ilikwishaondolewa tangu mwaka 2000, Kamati inakubaliana na marekebisho katika kifungu cha 116.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na marekebisho yanayopendekezwa katika vifungu 104, 107 na 114 vinavyokataza uvaaji wa sare katika maeneo ya uchaguzi na kumpa madaraka mkuu wa uchaguzi kumwondosha katika daftari mtu yeyote ambaye atapatikana na hatia kwa makosa ya rushwa katika uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, sheria ya pili inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Uchaguzi katika Serikali za Mitaa namba 4 ya 1979. Marekebisho yanayofanyika katika sheria hii yanakusudia kuleta uwiano katika taratibu za kuandikisha wapigakura katika daftari la kudumu la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Madiwani. Kama nilivyoeleza hapo nyuma, sheria hii kama ilivyo sasa haitoi kabisa mamlaka ya fursa kwa Tume kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa madiwani. Aidha, yapo maeneo mengine ambayo marekebisho yake yanafanana na yale yaliyofanyika katika Sheria Namba 1 ya 1985.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 48 kinafanyiwa marekebisho ili muda uliopo wa kufanya uchaguzi mdogo wa Diwani baada ya uteuzi wa wagombea uwe siku 30 badala ya siku 60 hadi 90. Kama ilivyo kwa upande wa chaguzi ndogo za Wabunge, Kamati yangu inakubaliana na marekebisho haya kwani tunaamini kuwa yataiwezesha Tume ya Uchaguzi kufanya chaguzi ndogo katika muda mfupi zaidi kuliko ilivyo sasa, ikizingatiwa kuwa eneo la Kata ni dogo kuliko Jimbo. Vile vile, kifungu cha 48 kinafanyiwa marekebisho ili kuweka sharti kwa wagombea wanaojitoa katika uchaguzi kula kiapo kwa ajili hiyo mbele ya Hakimu. Kama ilivyo katika rekebisho la uchaguzi wa Bunge, Kamati inakubaliana na marekebisho haya katika uchaguzi wa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nitoe maoni machache kuhusiana na maeneo yafuatayo ya Muswada huu: -

(i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi iwe makini katika kuhakiki umri wa raia ambao hawajafikisha miaka 18 wakati wa kuandikisha, lakini watafikisha miaka 18 siku ya kupiga kura kabla ya kuwaandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura ili kuondoa udanganyifu.

(ii) Ili kuzuia vitendo vya upendeleo vya kisiasa, maafisa wanaopewa dhamana ya usimamizi wa upigaji kura ambao ni wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji wapewe adhabu inayolingana na uzito wa kosa lenyewe endapo watakiuka taratibu za upigaji kura. Kamati inaamini kuwa utaratibu huu utasaidia kuleta amani nyakati za uchaguzi na kuimarisha demokrasia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa maoni ya Kamati. Napenda pia kuwashukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge na wasaidizi wao kwa umakini wao katika

kuleta marekebisho haya ambayo tunaamini yatachangia kwa kiasi kikubwa kuendeleza na kuimarisha demokrasia ya uwakilishi hapa nchini.

Napenda kuwashukuru Wajumbe wenzangu katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala waliozipitia kwa makini sheria hizi na kutoa mchango mkubwa ulioboresha Muswada huu. Aidha, nawashukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Aggrey Nzowa, kwa ushauri na huduma mbalimbali walizozitoa kwa Kamati hii wakati tunaupitia Muswada.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wadau kutoka Vyama vya Siasa kwa maoni yao ingawa hapo mwanzoni walitupa shida sana kwa kutokuelewa majukumu ya Kamati za Bunge, lakini baada ya kuwaelimisha walituelewa na kwa kweli wamechangia mchango ambao tumeweza kuuhusisha katika maoni yetu. Mwisho, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza

Mheshimiwa Spika, sasa kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naiunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI NA MSEMAJI MKUU KWA OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu namba 43(5)(c) kama maoni yetu kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi *(The Electoral Laws Act, 2004)*.

Pia, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kumaliza shughuli za Kamati salama na kuwatakia kila la kheri kwenye ngwe ya zaidi ya miezi miwili ya kujadili Bajeti ya Serikali.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena kurudi Bungeni na tunamshauri afanye kazi nzuri na ya ziada ya kusukuma mabadiliko ya kidemokrasia huko huko alikohamia kwa kuiga mfano wa akina Laira Odinga wa Kenya ambao walijiunga na Chama Tawala na kisha dakika za mwisho wakakimbia na kuuimarisha Upinzani na kuuletea ushindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali hatimaye imekubali hoja ya Vyama vya Upinzani ya kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapigakura kama ilivyoainishwa na Katiba yetu ya nchi. Wasiwasi wetu ni muda uliobakia kabla daftari hilo kutumika iwapo utatosha katika maandalizi na hasa tukiangalia *experience* ya nchi nyingine zilizofanya zoezi hilo, mfano nchi ya Kenya ilitumia zaidi ya miaka mitatu kufanya maandalizi hayo.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wakati wote kukubali kufanya marekebisho ya uendeshaji chaguzi zetu kwa misingi ya kuzingatia mabadiliko makubwa yanayotokea duniani na hususan ndani ya jamii yetu kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tukijifanya kwamba hayatuhusu au kufanya marekebisho huku tukiwa tumezugwa na hila zilizojificha kindani ndani, mtafaruku unaweza kuja kufumuka katika namna ambayo huenda tukashindwa kuukabili.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi siyo jambo la kuchezea au kufanyia masihara. Kwenye baadhi ya nchi mitafaruku iliyotokea au inayoendelea kutokea imesababishwa na kuwa na taratibu au sheria mbaya za kuwapata watawala au viongozi wao. Nyingi ya sheria hizo na taratibu zinakuwa zimetungwa na kupitishwa kimakusudi kwa ajili ya kuwasaidia wale walioko madarakani, matokeo yake ni kama ambavyo tumekuwa tunashuhudia vifo vya raia, mapambano ya raia na vyombo vya dola, uanzishwaji vikundi vya uasi vyenye silaha na kwenye nchi nyingine umma usioridhishwa na matokeo ya chaguzi umediriki hata kufanya maandamano makubwa ya kupinga chaguzi na kuvamia majengo ya watawala na kuwatimua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa minajili ya kudumisha umoja wa kitaifa ambao tumekuwa nao tangu uhuru, hali ya amani na utulivu ambayo imetujengea heshima dunia nzima si vema mambo haya tukayaachia yakaporomoka kwa kuruhusu au kupitisha sheria na taratibu mbaya za uchaguzi ambazo zinaangalia malengo ya muda mfupi, ya watu wachache au kuwajengea wigo walioko madarakani ili watawale daima. Sheria na taratibu za namna hiyo hazitatujengea mazingira endelevu ya udumishaji amani na utulivu na yenye kuwaondolea umaskini Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaomba kuainisha baadhi ya mapungufu kama tulivyoyabaini ndani ya Muswada uliowasilishwa na Serikali, Kifungu kipya cha 7(a) kinaongezwa ili kuwafanya Wakurugenzi wa Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Mji na Wilaya kuwa maafisa waandikishaji wa wapigakura katika Majimbo ya Uchaguzi.

Kifungu hiki watu wote waliopewa mamlaka ni watumishi wa Serikali ambao wako chini ya TAMISEMI. Mkubwa wao ni Mwenyekiti wa Chama Tawala na Waziri wa hiyo Wizara ni kiongozi mkubwa katika Chama Tawala. Kwa mantiki hiyo, haki inawezaje kutendeka? Ndiyo maana tunashauri na kusisitiza Tume itumie watu wake katika zoezi zima la uandikishaji. Iwapo imeamua kuwatumia basi ni bora kila mhusika aingie mkataba na Tume kama mtu binafsi na siyo kama Taasisi au nafasi aliyonayo mtu katika Taasisi husika.

Hali ilivyo hivi sasa na kwa kuzingatia hali halisi ambayo tumeendelea kuishuhudia katika chaguzi ambazo zimefanyika watumishi hawa ambao wako chini ya TAMISEMI kwa mfumo wa kiutawala tulionao kwa vyovyote vile wataendelea kufanya kazi kwa kuzingatia maelekezo ya mabosi wao na hata kupokea lugha ya vitisho kama ambavyo imekuwa ikifanyika, mfano eti *DC* atakayeruhusu upinzani kushinda katika eneo lake atakuwa amejifukuzisha kazi. Lazima Serikali ikubali kwamba demokrasia ina gharama zake na gharama hizo za kidemokrasia ndizo zinazoiwezesha kuwepo madarakani na kuiwezesha kuyafanya mengine yote yanayopangwa kufanyika. Hoja ya Tume ya Uchaguzi kuwa na watumishi wake bado ni ya msingi na inabidi izingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 cha Muswada huu kinachoongeza kifungu kipya 11(8) kuhusu utunzaji wa daftari la awali la wapiga kura kwamba likae sehemu za wazi, Kambi ya Upinzani haina tatizo na hilo ila inapendekeza kuwa kutokana na kukua

kwa teknolojia takwimu za uandikishaji za wapiga kura ziwekwe kwenye tovuti, kitu kitakachosaidia kwa mtu yeyote mwenye nia na lengo la kuangalia takwimu za sehemu yoyote ya nchi yetu ili aweze kuzifanyia ulinganifu na takwimu za idadi za watu katika eneo analolihitaji aweze kufanya hivyo na siyo mpaka aende Ofisi za Tume au kusafiri mpaka eneo husika.

Aidha, kuweka takwimu hizo kwenye tovuti kunatoa mwanya wa demokrasia ya uwazi, njia inayoonyesha kuwa nchi yetu inakomaa kidemokrasia, udanganyifu unaoweza kujitokeza unaweza ukazuiwa. Vile vile, ushirikishwaji wa asasi tofauti zinazoitakia mema nchi yetu zitapata fursa ya kushiriki kutoa maoni na kufuatilia uchaguzi wetu na zoezi zima la uandikishwaji. Tunaipongeza Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar *(ZEC)* kwa kuliona hilo na kukubali utaratibu wa kuweka takwimu zote za uchaguzi kwenye tovuti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10 cha Muswada huu kinachorekebisha kifungu cha 12(2) kinachompa mamlaka Mkurugenzi wa Uchaguzi kuhifadhi na kufanyia marekebisho Daftari la Kudumu la Wapigakura, Kambi ya Upinzani inauliza kwa kuwa Tume ya Uchaguzi ni ya kudumu na mawakala na waandikishaji siyo wa kudumu, wakati wa kufanya marekebisho mawakala wa vyama watakuwepo? Je, Vyama vya Siasa kama siyo hivyo vitawakilishwaje? Tutaomba majibu kutoka kwa Serikali.

Tunapendekeza kuwa sheria itamke wazi jinsi ya kushirikisha wadau vikiwemo Vyama vya Siasa katika zoezi la kufanyia marekebisho kwenye daftari la wapiga kura badala ya kumuachia Mkurugenzi wa Tume kufanya marekebisho hayo peke yake.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 cha Muswada kinarekebisha kifungu cha 12(a) cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 kwa kuongeza kifungu kidogo cha pili ili kuiwezesha Tume kuwa na mamlaka ya kuandikisha wapiga kura waliopo Zanzibar wanaostahili tu kupiga kura katika uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hii inajikanganya na tafsiri ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani kuna Wabunge wa Muungano waliopo Zanzibar ambapo pia sheria hii hairuhusu kuwapigia kura kama Rais wa Muungano anavyopigiwa kura na watu ambao siyo Wazanzibari. Sheria hii itakuwa inawanyima haki Watanzania waishio Zanzibar kwa kutopewa fursa ya kuchagua Wabunge na Madiwani wao.

Mheshimiwa Spika, sheria hii pia haijafafanua utaratibu wa kuandikisha kupiga kura kwa Watanzania waishio nje ya nchi. Tunapendekeza sheria iweke utaratibu wa kuandikisha Watanzania waishio nje ya nchi ili waweze kuwapigia kura viongozi wao kwa kutumia *internet* au Balozi zetu za nje kama nchi nyingine zinavyofanya.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13 cha Muswada huu kinarekebisha kifungu cha 15 cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 ili kuiwezesha Tume kupanga muda wa uandikishaji na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura. Kutokana na sheria kutotamka bayana muda wa uandikishaji na kuachia Tume kuchagua na kuweka muda wa mwisho wa uandikishaji ni kitu ambacho kinaweza kutumiwa vibaya na baadhi ya watendaji. Tunashauri sheria iweke bayana muda wa uandikishaji ili kuondoa

ubabaishaji unaoweza kutumiwa na baadhi ya viongozi kuwanyima Wananchi haki zao za msingi za kushirikishwa katika Daftari hili la Kudumu la Wapigakura.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6 (4)(c) kilifanyiwa marekebisho kuhusu *voters education* kama ninavyokinukuu: *"The Commission shall be responsible for providing voters' education throughout the country and shall coordinate and supervise persons who conduct such education."*

Kambi ya Upinzani inaona hilo kwa Tume ya Uchaguzi ni kitu kizito mno, kwanza ukubwa wa eneo wa nchi yetu siyo rahisi kwa Tume kufanya kazi hiyo au kuisimamia peke yake. Aidha, tunapendekeza kuwa Tume iwezeshe Vyama vya Siasa katika kutoa elimu hiyo kwani vyama ndivyo vilivyo karibu na Wananchi. Vile vile, vyama vina programu zao kwenye suala zima la elimu ya upigaji kura na programu hizo zinatofautiana. Sasa kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu na vyama kufanya shughuli zake kwa kutegemea programu zake, bado tuna wasiwasi na suala ambalo Tume ya Uchaguzi imejivisha ya ku-*supervise* na ku-*coordinate* kwamba kazi hiyo itafanyikaje, tutaomba ufafanuzi kutoka kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, maneno ya *supervise persons who conduct such education* yanaleta utata kwani inaonyesha kuwa Tume imeshaandaa mitaala itakayotumika kutoa elimu, kitu ambacho kinaweza kuleta mtafaruku kwa wananchi na badala ya kutimiza malengo ya elimu ya wapigaji kura, ikaleta kitu ambacho hakikutarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kifungu kinachozungumzia mgombea kujitoa, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuongezwe kipengele kitakachowabana watu wa namna hii ambao wanajitoa wakati ambapo taratibu na maandalizi ya chaguzi yamekamilika. Wakati wanapojitoa huwa tayari pesa nyingi zimetumika kwa upande wa Tume na kwa upande wa Vyama. Ili kuwadhibiti na wakati mwingine kuzima tamaa zao za kupokea pokea hongo ni budi watu hawa wafungwe miaka mitano jela, faini isiyopungua shilingi milioni 5 na kuzuiwa kugombea uongozi wowote wa kiserikali kwa kipindi cha miaka 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili nami niweze kuchangia kwenye Muswada huu. Lakini awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge wa Bariadi Mashariki kwa tiketi ya CCM kwa ushindi wake mkubwa na uliofanya Chama Tawala kuongeza nguvu yake ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu wa uanzishaji wa daftari la kudumu la wapiga kura. Kwa ujumla naunga mkono uanzishaji wa daftari hilo. Hata hivyo, ninazo *reservations* chache ambazo nataka nitoe. Kwanza kabisa ni *timing* au ni wakati gani ambao tumedhamiria kuleta daftari hili la kudumu.

Mheshimiwa Spika, nalisema hivi kwa sababu nina wasiwasi kwamba daftari hili la kudumu ambalo linaanzishwa kabla ya vitambulisho vya Taifa kuanzishwa kama litaweza kwa kweli kukidhi haja ya kudhibiti upigaji kura kwa watu ambao si Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukizungumza sana muda mrefu kuhusu kuwepo kwa vitambulisho vya Taifa *(National Identity)* na kutokana na vitambulisho vya Taifa uanzishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura lingekuwa ni rahisi zaidi. Kwa sasa hivi tutatumia fedha nyingi sana kuanzisha daftari hili na nina wasiwasi kama kutakuwa na uangalifu mkubwa katika kuhakikisha kwamba wanaojiandikisha katika daftari hilo la kudumu wote kweli wanastahili kwa umri na kama kweli ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu katika uandaaji wa vitambulisho vya Taifa mambo mengi sana yanaangaliwa. Mpaka sasa kuna malalamiko maeneo mengi kwamba wapiga kura wengine si Watanzania. Ni namna gani tutawadhibiti hawa wasijiandikishe kwenye daftari hili kama ile *process* nzima ya kuanzisha vitambulisho vya Taifa itakuwa bado. Nchi zingine nyingi ambazo zimeanzisha madaftari ya kudumu ya wapiga kura kwanza yanakuwa na vitambulisho vya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nimekuwa mwangalizi mzoefu kwa muda mfupi, nimeangalia uchaguzi wa Kenya mwaka 2002, uchaguzi wa Rwanda mwaka 2003 na uchaguzi wa *South Africa* mwaka 2004 na hasa Kenya na Afrika Kusini unaona kwamba vile vitambulisho vya Taifa ndiyo vinasaidia, vinaweka *base* nzuri ya kutengeneza lile Daftari la Kudumu la Wapiga kura. Sasa hivi kitakachotokea ni kwamba kutakuwa na Watanzania ambao watakuwa na kadi za kudumu za kupiga kura na si ajabu wataonekana kwamba ni Watanzania bora kwa sababu angalau wana vitambulisho vya kupigia kura. Mwingine ambaye hatakuwa na ari ya kupiga kura na kwa hiyo, hakwenda kujiandikisha atakuwa bado hajijui kwamba ni Mtanzania kiasi gani. Mpaka pale unapokuwa na moyo wa kwenda kupiga kura ukajiandikisha, hapo ndipo unaweza kuwa na kadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nasema kuna upungufu kwa sababu kitambulisho cha Taifa na kama kikiandaliwa vizuri kinaweza kikakidhi kabisa haja hii. Inawezekana kumekuwa na *pressure* kwamba lazima tuwe na daftari hili la kudumu kabla ya mwaka 2005. Kwa bahati mbaya nahisi kwamba *pressure* zaidi imekuwa ya kutoka nje badala ya kutoka ndani.

Pamoja na kwamba ni jambo muhimu, lakini maandalizi yangefanyika na kwa sababu uandaaji wa vitambulisho vya Taifa unaweza ukaenda pamoja na uandaaji wa Daftari la Kudumu, hili lingekwenda sambamba na lingepunguza gharama kwa sababu mabilioni yatakayotumika kuandaa daftari la kudumu. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekuwa ikizungumza kwamba maandalizi yapo ya kuandaa vile vile vitambulisho vya Taifa, yangewekwa pamoja masuala haya mawili tungepunguza gharama kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba labda ingewezekana kufikia mwaka kesho tungekuwa hatujawa tayari kuwa na vitambulisho vya Taifa na kuwa na daftari la kudumu, lakini angalau tungekuwa na uhakika kwamba tunafanya kitu ambacho hatutarudi tena nyuma kujaribu kurekebisha. Nina hakika tutakapoanza kutayarisha vitambulisho vya Taifa tutakuta kwamba kuna mambo tumekosea au kuna wengine waliojiandikisha kwenye daftari la kudumu ambao siyo Watanzania na itabidi turudi tena upya kurekebisha kwa kiasi kikubwa lile daftari la kudumu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo siyo mwanzo mbaya, mimi ilikuwa ni wazo langu tu kwamba kweli vitambulisho vya Taifa lazima tujielekeze kwa nguvu zetu zote tuwe navyo na vitatusaidia katika masuala yote hayo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia kuhusu Muswada huu ni kuhusu Mahakama za Uchaguzi. Katika nchi zingine tunaona kwamba kuna Mahakama Maalum za Rufaa za Uchaguzi *(Electoral Courts of Appeal)* na hizi zinafanya kazi kwa muda ule uliokuwa umewekwa, kama kuna matatizo na malalamiko basi yanapelekwa kwenye mahakama hiyo mahsusi na siyo hizi mahakama za kawaida kwa sababu kuchanganya kazi za kawaida za mahakama na kazi za malalamiko ya chaguzi inachukua muda mrefu sana kesi za chaguzi kumalizika.

Sasa tungetenga kabisa tuwe na mahakama maalum kwa kipindi kile kama ni cha miezi sita cha kutoa malalamiko, kipindi kile tunaunda mahakama maalum za chaguzi katika ngazi zote za Taifa na Wilaya. Hili litaondoa malalamiko ya kesi za chaguzi kuchelewa sana kushughulikiwa na masuala kama hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, nipongeze Muswada hasa pale ambapo imeelezwa kwamba Tume ya Uchaguzi itakuwa na jukumu na itawajibika kwa kweli kueneza elimu kwa wapiga kura. Nitofautiane na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba jukumu hili lisiwekwe kwenye Tume ya Uchaguzi. Kwa kweli jukumu hili ni la Tume ya Uchaguzi, lakini ni kweli kwamba *resources* zitatakiwa za kutosha kwa sababu ni suala ambalo ni zito linahitaji *resources* siyo tu watu, lakini vile vile fedha nyingi, lakini litasaidia.

Mheshimiwa Spika, ukiona uzoefu uliopita, vyama na wagombea ndiyo walikuwa wanahamasisha watu waende wakajiandikishe kupiga kura na baadaye wapige kura, wakati ambapo kwa kweli ni jukumu la Tume ya Uchaguzi kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanajiandikisha na wanapiga kura. Ukiachia vyama sana sana watakuwa wanawatafuta wale wapenzi wa vyama vyao ndiyo wajiandikishe na wapigie kura chama chao.

Kwa hiyo, kwa Watanzania ambao labda hawana vyama na huwezi ukamfuata ukamwambia jiandikishe maana ukimlazimisha kujiandikisha kumbe labda hakupigii kura kama huna hakika kwamba ni mshabiki wa chama chako. Lakini Tume ya Uchaguzi yenyewe kwa sababu itakuwa inazungumzia upigaji kura kwa Watanzania wote bila kujali yule ambaye ni mwanachama wa chama hiki au kile kutakuwa na *impact* kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha elimu hii ya wapiga kura si kweli tu kwamba njia inayotumika ni lazima uende moja kwa moja kwa wapiga kura, hiyo ni moja. Lakini kutumia kwa kiasi kikubwa sana mabango, kutumia kwa kiasi kikubwa sana redio ambazo zinafika kila mahali nchini, *television* kuna mahali bado, lakini wananchi walio wengi sasa hivi wanaangalia *television,* magazeti, mambo yote haya unaweza kutoa elimu kwa njia hiyo. Kwa hiyo, elimu nyingine inaweza ikatolewa pale pale Makao Makuu ya Tume ya Uchaguzi kwa kutumia vyombo hivi ambavyo nimevitaja. Lakini vile vile mikutano.

Mheshimiwa Spika, juzi tulipokuwa Afrika Kusini tuliona Tume ya Uchaguzi ikiwa na mpango unaitwa *Road Shows,* wanafunga barabara au eneo la labda kwenye kiwanja na wanaonyesha mambo mbalimbali, lakini nia kubwa ni kuhamasisha watu wapige kura. Wana michezo mbalimbali, utamaduni, wanakuwa na maigizo mbalimbali katika kueleza nia ya uzuri wa kupiga kura ili uweze ku-*exercise* demokrasia yako. Sasa mambo kama yale hayaonekani sana huku. Mikutano ya hadhara tunayofanya ni ya vyama, lakini kumbe mikutano ya hadhara inaweza ikafanyika na Tume ya Uchaguzi kwa nia ya kueneza elimu ya kupiga kura. Kwa hiyo, hili naliunga mkono na ningeomba kwa kweli liangaliwe kwa sababu *resources* nyingi sana zinatakiwa, lakini ni jambo ambalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ningeomba, nimeona kidogo kwenye Muswada kwamba kutakuwa na mkutano wa wagombea na hasa kinachoongelewa zaidi pale ni kuhusu wakati ule wa kampeni kuhusu programu zao za kampeni kwamba zisigongane, kwa hiyo, kutaitishwa mkutano wa wagombea na vyama. Lakini ilitakiwa kuwepo na Kamati maalum na ionyeshwe kwenye sheria kwamba Kamati za Ushauri za Vyama vya Siasa *(Party Liaison Committee - PLC)* mahali pengine. Kamati hizi zinakutana kila wiki kwenye ngazi ya Wilaya na ngazi ya Taifa ambako Vyama vyote ambavyo vinagombea vinaitwa pale, kila mmoja anatoa duku duku lake kwamba naona chama hiki kinaleta *rough* katika uchaguzi, mnazungumza, mnasuluhisha, mnashikana mikono, inaleta umoja na uelewenо katika uchaguzi na kuondoa chuki na hamasa hizi ambazo zinaweza zikajitokeza wakati wa kampeni. Kwa kweli *Party Liaison Committees* ni muhimu sana kwani wote ni Watanzania, tunachotaka ni demokrasia tuweze kupata viongozi halali. Kwa hiyo, mnapokutana inakuwa ni vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pale Ukonga, nikuhakikishie kwamba mwaka 2000 nimemaliza kampeni bila hata kumwona mgombea aliyenifuatia wa CUF kwa kura kwa sababu kulikuwa hakuna *Party Liaison Committee* kwamba tukutane wagombea tuwekwe pamoja pale na Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya, kwamba nyie ni wagombea bwana kuna *rough* hivi na hivi tunatakiwa tufanye hivi, hakuna, hili ni suala ambalo ni muhimu tulifanye ili kuleta mshikamano ndani ya Watanzania wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Spika, la mwisho limezungumziwa hili la watu walioko nje kupiga kura. Hili ni suala muhimu na nadhani lipo kwenye sheria kuu, sasa utekelezaji wake kwamba tuna litekeleza vipi ni muhimu ili Watanzania walioko nje kikazi siyo mtu aliyesafiri lakini aliyetumwa ubalozini na shughuli zingine za kitaifa waweze kupata

nafasi ya kupiga kura. Lakini katika kuwezesha Watanzania hata ambao wana upungufu kwa mfano wazee sana, akinamama wajawazito na vilema kwenye sheria tungewatengea muda maalum au siku maalum ya kupiga kura kama wanavyofanya wenzetu. Hii itawapa hawa watu ambao hawana uwezo wa kuhimili mikiki mikiki ya siku ya uchaguzi ambapo kuna vurugu na foleni ndefu na kuchoka, wazee wengine wanaanguka chini, vilema, baadaye wanaamua wasipige kura kumbe wangeweza kupiga kura kwa sababu wana haki. Mzee hata wa miaka 100 bado ana haki ya kupiga kura.

Kwa hiyo, tumpe nafasi hiyo kwa kumtengea siku maalum ikiwezekana na mpangilio uwe ni mzuri. Hii itawezesha kwa kweli watu wengi kupiga kura. Wengine wanapofanya hivi ndiyo unakuta kwamba asilimia kubwa ya wanaostahili kura wanapiga kura, wanapiga kura. Asilimilia karibu 75 au 80% ya wanaostahili kupiga kura Afrika Kusini wanapiga kura. Sisi hapa ni asilimia karibu 60, 65% tungeweza kuiongeza kama tungeweka mazingira mazuri ya watu wote kupiga kura hata wale vilema ambao wanaweza hata kufuatwa hata nyumbani wakapigia kura nyumbani, wazee sana, wajawazito na watu kama hao. Sasa haya bila kuwekwa kwenye sheria kwa kweli haitawezekana na mwisho wa siku utaona kwamba hawapigi kura.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema ni mwanzo mzuri, tuanzishe daftari hilo, lakini kwa kweli tuangalie kwamba kufika mwaka 2010 basi tuwe na vitambulisho vya Taifa ambavyo vitatumika sasa kurekebisha daftari ambalo tutakuwa tumelianzisha mwaka huu kwa sababu naamini baada ya vitambulisho vya Taifa kutakuwa na haja ya marekebisho makubwa kwenye daftari hilo tutakalokuwa tumelianzisha. Lakini mwanzo ni mzuri kwa hiyo, naunga mkono na kwa hiyo, nilitaka niyaseme hayo.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Ni vizuri kuzungumzia matatizo yote ya uchaguzi lakini kanuni yetu inataka tuzungumzie Muswada uliopo mbele yetu. Kwa hiyo, naomba wasemaji wajielekeze kwenye *provisions* za Muswada.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kujadili marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi kuwezesha kuanzishwa kwa daftari la kudumu la kitaifa la wapiga kura kwa kurekebisha sheria zetu mbili, Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na ile ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1979.

Niishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushughulikia na hatimaye kutuletea Muswada huu wa mapendekezo haya Bungeni ambayo ni muhimu sana kwa chaguzi hizi mbili zijazo wa Novemba wa Serikali za Mitaa na ule wa Oktoba mwakani. Nafikiri nia ni kufanya uchaguzi uwe wa haki zaidi na kupunguza malalamiko ambayo hayana sababu wala mwelekeo. Napenda kuwapa salaam za rambirambi Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba mkubwa walioupata wa baba yao mzazi. Pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge wa Bariadi Mashariki kwa kurudi tena kwa kishindo hapa Bungeni. Mimi naamini hajarudi hapa kama Raila, ila inampa nafasi nzuri

zaidi sasa ya kufanya kazi yake ya Ubunge maana kuna tofauti kubwa sana ukiwa katika benchi lipi katika kuchangia hapa Bungeni na kuwa Mbunge bora zaidi kwa wananchi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninafuatia kuzungumza baada ya kuongea Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, ambaye ameshapata fursa kadhaa za kwenda Kenya, Rwanda na *South Africa* kwa hiyo, tayari ana uzoefu mkubwa wa hapa hapa nchini na nchi hizo zingine. Basi nikuombe Spika sasa kwa uchaguzi wa Angola unaofuata kwa sababu hawa jamaa walikaa sana kwetu Kongwa tukaone demokrasia yao inafananaje na mimi iwe zamu yangu kwenda kuona uchaguzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima wananchi waone kuwa Madiwani, Wabunge na Serikali yao kwa kweli wanatokana na ridhaa yao. Lazima Serikali i-*enjoy highest level of legitimacy* kutokana na wananchi. Tunachokifanya hapa leo ni kutekeleza hilo la kuelekea kwenye kuwa na chaguzi ambazo ni bora zaidi na za wazi zaidi. Jambo kubwa ambalo nilikuwa nimejiandaa kuzungumza na kwa ajili ya kuokoa muda wako lilikuwa ni hili la kufanya maandalizi ya kuandikisha raia wetu kwa kuwa na vitambulisho vya kitaifa kabla ya zoezi hili.

Lakini kwa kuwa Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, amekwisha lieleza kwa undani na *points* zangu zote karibu ameninyang'anya kwa hiyo, hilo mimi sitalizungumza ila nitalisisitizia tu kwamba nalo liangaliwe, tunajua kwamba ni gharama kubwa lakini litazamwe kwa sababu kiutaratibu hilo ndiyo linatangulia. Mtu atambuliwe kwanza kwamba ni raia halafu kwa kutumia kigezo kile cha uraia wake ndiyo ataandikishwa. Lakini kwa sababu zilizoelezwa na uchaguzi ni mwakani na kuna mambo ambayo yanatakiwa yarekebishwe hapa na pale kwa kweli ni lazima hivyo ambavyo Serikali imeona busara lifanyike.

Zoezi hili la uandikishaji wapiga kura ni gharama kubwa sana. Kambi ya Upinzani, walikuwa wamependekeza kile kipengele kinachosema kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri, Mitaa, Majiji ndiyo wasimamie daftari lile kwa maana ya uandikishaji kwamba si sahihi, ningeomba nitofautiane nao. Kwa vile sasa Tume inapewa kazi nyingi zaidi za muda wote zaidi. Kazi za *registration* watafanya wao, za *maintenance* za hiyo *register* ku-*up date* hiyo *register* mara kwa mara, ku-*issue voter cards,* ku-*replace* zile zilizopotea kwa hiyo ni kazi muda wote.

Sasa ukisema hawa wasihusike, hao wengine utawatoa wapi? Utaweza kweli kuajiri watu wote hawa nchi nzima kila mahali wafanye hii kazi? Kumbuka katika nchi yetu bado tuna upungufu mkubwa sana wa waganga, walimu na kada nyingine nyingi. Sasa tuanzishe tena kada nyingine itakayotumia gharama kubwa kwa kazi hii, mimi nafikiri burasa iliyotumika kwa pendekezo hilo la Serikali kwamba hawa waliopo wafanye kazi hiyo, nadhani ni sawa sawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mazuri ambayo ningependa nipitie mawili, matatu kwa haraka tu.

Moja ni lile la Tume kupewa jukumu pale kifungu 4 (c) *section 6* la kutoa elimu kwa wapiga kura, kwa sababu ilikuwa ni moja ya vurugu kubwa huko nyuma kwamba kila mtu au *NGO* au asasi mbalimbali zilikuwa zinakwenda kwa maana ya kutoa elimu kwa wapiga kura, lakini badala ya elimu ile ikawa inatafsiliwa kama vile ni kumpiga vita Mbunge aliyeko au kupiga vita Chama Tawala kilichopo pale. Sasa Tume kupewa fursa hii ya kuratibu utaratibu huu ni nzuri sana naiunga mkono itaturahisishia kutoa elimu ambayo kwa kweli inahitajika kwa wapiga kura wetu ili waweze kupiga kura ipasavyo.

Vile vile kile kifungu ambacho kimependekezwa hapa kinachowataka wagombea wa Urais kufanya *statutory declaration* mbele ya Jaji kuhusiana na taarifa zao ni muhimu sana. Litatusaidia sana ili katika ofisi hiyo muhimu sana tusije tukapata watu ambao wamekwenda kule na taarifa ambazo kumbe labda hazikuwa sahihi sana. Hiki kifungu ni muhimu nakiunga mkono, kinatutakia mema katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kile kifungu cha kufanya rufaa badala ya kwenda kwenye Mahakama za Mkoa ziwe kwenye Mahakama za Wilaya itapunguza sana usumbufu na gharama kwa chaguzi zetu zilizo nyingi. Nitofautiane na mawazo yaliyokwishatolewa ya kuhusu habari za waandikishwaji kuwa *floated* kwenye tovuti.

Baadhi ya habari zinaweza zikawa *floated* lakini siyo *information* zote. Tukifika mahali *information* zote za watu wanaandikishwa inaweza ikawafanya baadhi ya watu wasipenda kuandikishwa kwa sababu kuna ile *right* ya *privacy* ya mtu. Kwa hiyo, Tume iangalie ni mambo gani inaweza ikaya-*float* huko kama itakubaliana na suala hilo kama Serikali itakubali, lakini mimi nasema kama itakubaliana basi baadhi ya *information* ndizo ziende huko lakini si zote hasa takwimu hizi zinaweza kuwa *floated* kule.

Mheshimiwa Spika, mwisho basi nitoe mapendekezo kama nilivyosema toka mwanzo siyo nia yangu kuchukua muda mwingi, lile suala la vitambulisho vya kitaifa tulivyosema tungependa kulisisitizia, nikubaliane kabisa na hili ambalo Kambi ya Upinzani, wamelisema na mimi nilikuwa nimeliandaa kulizungumzia la wagombea ambao ni kama wasumbufu. Mtu anagombea, Tume inachapisha inaingia gharama kubwa, dakika za mwisho anajitoa kwa sababu ambazo hazieleweki. Ni vizuri sheria hii ikajaribu kuangalia watu wa namna hiyo, kukawa na faini fulani au kitu fulani kinachozuia tabia ya aina hii kwa sababu ni usumbufu mkubwa sana na ni gharama kubwa sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Niseme kwamba tatizo si tu peke yake kuandikisha wapiga kura ambao tunalitatua kwa kupitisha sheria hii, lakini vile vile ni kuwezesha walioandikishwa kupiga kura hasa vijana wetu wengi hawapigi kura. Kwa hiyo, hili nalo litafutiwe dawa tufanyeje ili waweze kupiga kura ndugu zetu hawa hasa vijana pamoja na yale makundi maalum ambayo Mheshimiwa Dr. Mahanga, amechangia hapa ya wazee na wengine ili kuhakikisha kwamba wanaitumia demokrasia yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nisema kwamba mabadiliko yote haya yataiongezea Tume ya Uchaguzi uwezo wa kufanya kazi yake *more professionally* na kuwa *more effective.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sheria hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nami nachukua fursa hii kuwapa pole wote Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na ndugu zao. Nampongeza Mbunge mpya, Mheshimiwa Danhi Makanga. Mpya kwa maana ya Chama cha Mapinduzi kwa kushinda kwa kura hizo. Baada ya hayo natanguliza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho ninataka kukichangia au kukielewa kuhusu hili daftari la wapiga kura. Kwanza hili daftari la wapiga kura wananchi ambao wanatakiwa kujiandikisha hivi sasa mpaka hapa tulipo wanaelewa kitu chochote? Ikiwa mimi Mbunge nimeelewa asilimia 50 kwa 50, sikuelewa vizuri mpaka sasa nini kitatokea katika uandikishaji wa daftari hili? Kwa sababu daftari la wapiga kura hivi sasa katika nchi yetu tuna nchi mbili, tuna nchi moja ya Tanzania Visiwani, tuna nchi moja ya Tanzania Bara, kwa pamoja inakuwa nchi moja.

Wakati wa kuandika daftari hili la wapiga kura najua watu wengi watajiandikisha, walio hapa Tanzania Bara, watakwenda Tanzania Visiwani, kujiandikisha kule na wakirudi huku watajiandikisha kwa sababu wanayo haki. Lakini je, itajulikanaje au itafahamikaje kwamba mtu huyu amejiandikisha mara mbili ili asipate nafasi ya kupiga kura mara mbili? Kwa sababu wengine wanajiandikisha halafu kadi watakayopewa wanaacha kule kule alikojiandikisha mfano kajiandikisha Tanzania Visiwani, kajiandikisha na Tanzania Bara, kadi ataacha kule Zanzibar ili ampe mtu siku ya uchaguzi akapige kura. Je, daftari hili litagunduaje? Naomba kujua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, mtu aliyekwishajiandikisha katika daftari Mungu akajalia akamwita akafariki, kabla ya siku ya kupiga kura ni nani atakayefahamu kama mtu yule amefariki? Sisi kule Zanzibar tunaye Shekhe, Shekhe atakuwa na uwezo wa kufahamu watu wote waliojiandikisha mle ambao wamefariki? Je, kadi ile si itatumiwa vibaya? Daftari litagunduaje kwamba fulani amefariki? Hilo naomba Mheshimiwa Waziri anielimishe kidogo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni kwamba maafisa watakaoteuliwa kusimamia hili *book* watapatikana wapi? Je, hawana vyama? Watapatikana kutoka wapi, ambao watakuwa safi wasiwe wanapendelea upande wowote ama upinzani ama Chama Tawala. Watapatikana wapi wawe safi kwa asilimia mia kwa mia ili pasitokee mgogoro wote? Ni vigezo gani vitatumika? Ni watu gani watakaotumika ili pawe na amani katika kupiga kura? Kwa sababu sasa hivi amani ipo, lakini wakati wa kupiga kura amani itaondoka haizuru pana *book,* kila mtu atataka aendelee kutawala.

Mheshimiwa Spika, sisi CCM tunatawala maana na Wapinzani watataka watawale, hapo patatokea vurugu. Je, ni kitu gani Serikali imeshaweka kwa ajili ya kuwadhibiti hawa watu ambao waleta matatizo?

Jambo lingine ambalo nilitaka kuomba, kuna vijana wa shule wakati wa kujiandikisha umri wao utakuwa haujatimia, haizuru nimesikia hapa Mwenyekiti amesema kwamba wameomba kwamba waruhusiwe kujiandikisha ikiwa wamefikisha umri wa miaka 18. Siku hiyo ya uchaguzi patakuwa na nafasi ya kuwaingiza katika daftari wale? Si patakuwa na vurugu hii ambayo inakusudiwa kuondoshwa, wataingizwa vipi, hata na wao waweze kupiga kura? Naomba Mheshimiwa Waziri, anielimishe kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Tume ya Uchaguzi kwa kweli hapa ndiyo ninapokuwa na matatizo, huku Tanzania Bara kuna Tume ya Uchaguzi, Zanzibar kuna Tume ya Uchaguzi, Wabunge tunafuata taratibu za Tanzania Bara, lakini tunatoka Zanzibar.

Je, ni taratibu zipi zitatutawala sisi? Ni za kule Tanzania Visiwani au hizi za hapa ambazo zinazotayarishwa hivi ni zipi zitatutawala sisi ili pasije pakatokea matatizo. Daftari la wapiga kura hivi sasa kuna vyama tayari vimeshashinda hata daftari bado, daftari bado lakini kuna vyama fulani vinasema kwamba wao tayari wameshashinda. *(Makofi)*

Sisi CCM tunasema hawajashinda, wala hawatashinda. Narudia tena na sisi tunasema hawajashinda na wala hawatashinda. Je, Mheshimiwa Waziri, wenzetu hawa ambao tayari kabla ya daftari wameshaanza kutoa matokeo ya uchaguzi, je, daftari litatuambia nini kuhusu jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kusema hivi kwamba tunaomba Tume ya Uchaguzi baada ya taratibu nzuri walizokusudia kuzipeleka kwa wananchi, wasiache haraka haraka kutuelimisha. Sisi Wabunge na Madiwani na wananchi watuelimishe kuelewa vizuri ili pasitokee mgongano hasa huu upande mwingine ambao unataka lazima ushinde, sisi hatuna tatizo, tutashinda tu na tunaelewa taratibu zote zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba Tume ya Taifa ni lazima iwe makini sana na iwe na uwezo mkubwa iwape sheria ya kumudu mambo yao, pasipo na kuingiliwa. Maofisa watakaochaguliwa wawe waadilifu. Haizuru wataapishwa viapo, lakini kiapo unakula pale unapotaka kujitetea tu, unapotaka kufanya jambo unakipinga. Wawe waadilifu na wawe na uwezo mkubwa wa kufanya kazi na vile vile wasiwe wanapendelea upande wowote ili uchaguzi wetu uwe salama na amani.

*Book* la wapiga kura tunalikaribisha na sijui kama muda uliobakia utatosha kwa sababu hivi sasa hivi halijaanza na watu wapo wengi ambao wanataka kujiandikisha. Zanzibar watatumia *computer*, lakini mimi si mtaalam wa *computer. Computer* ikiwa mtu yuko nje hawezi kujiandikisha huko katika *computer* jina lake likatokea humu na yeye hakuandika huku Zanzibar?

Mimi najua kuipiga hivi hivi, lakini sijui utalaam ukubwa zaidi haitatokea matatizo hayo? Wenzetu Tanzania Bara, wanafanya vizuri maana hawaweki katika

*computer,* wanaweka tu pale orodha basi unajitazama pale. Kwa hiyo, mpaka yule afisa awe siyo mzuri ndiyo aweze kuingiza jina lake. Je, hayo hayatatokea?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri kwa hayo, machache anisaidie na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa jicho lako kuniona asubuhi hii na naomba nichukue nafasi ya awali kabisa kuungana na wenzangu kutoa pole za dhati kabisa kwa ndugu zetu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, wote wawili kwa msiba mkubwa walioupata. Naomba pia nimpe hongera ndugu yangu Danhi Makanga, kwa kurudi ndani ya Bunge. Suala ya namna ya kuja ni suala lingine lakini suala la kutumikia wananchi ni suala lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango kidogo kuhusu Muswada ulioko mbele yetu na naomba kwanza niseme kwamba napenda kurudia baadhi ya mambo kutokana na uzoefu ambao tumeupata kule *SADC* na ni juzi tu tumetoka *SADC* ambapo tumepokea taarifa ya wenzetu waliyokuwa wanatufanyia kazi ya kuangalia uchaguzi akina Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, pamoja na wenzetu. Kwa hiyo, kuna mambo ambayo kama *SADC* tunayawekea mkazo na ambapo hata sisi kama taifa pia tunapata sifa, ningependa kuyarudia hata kama *direct* hayapo kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kuligusia nianze tu kwa kutoa pongezi za dhati kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa jitihada inazofanya, pamoja na kwamba bado inaitwa kwamba siyo Tume Huru. Kuna wanaofikiri kwamba Tume Huru lazima isichaguliwe na Rais. Ukweli si hivyo hata nchi zinazotumia Tume Huru maana yake ni kwamba *consultation process* inaenda nje, lakini hatma ya yote, mteuzi wa mwisho ni lazima awe Rais. Sasa ndicho hicho ambacho tunakizungumza na hili si lazima liwe suala la Mheshimiwa Kiravu na Jaji Makame, hili nadhani ni la mhusika mwenyewe. Lakini tunachoomba hapa ni *National Process. (Makofi)*

Sasa hapa Tume imeleta kazi nzuri na nafikiri imejitahidi kufanya mawasiliano na wadau wote na kazi inayoletwa inaonekana iko *independent* na inalinda maslahi ya Taifa. Napenda kupongeza Tume kwa hili. Nimewasiliana na Tume mara nyingi katika sehemu mbalimbali nadhani Tume, inajaribu kuitikia kwenye yale ambayo tunawapelekea. Sasa naomba tu kwamba haya yote waendelee kuyakuza ili kujenga jina la Tume na huko nje Tume ya kwetu ina jina zuri na nafikiri iko *active* kwa kiwango cha kujenga amani na utulivu ndani ya taifa hili. Kwa hiyo, nadhani hili ni jambo la kwanza ambalo tunapaswa kulizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo nilitaka niligusie liko kwenye kifungu cha 7. Mimi nadhani tatizo la msingi katika kifungu hiki haipo katika nani afanye nini na ni watu gani. Mimi nadhani tatizo la msingi ni jinsi gani hawa watu watakuwa moja kwa moja wanawajibika kwa Tume yenyewe na kuacha kuwajibika kwa watu walio nje ya Tume katika kipindi cha uchaguzi. Kurugenzi kwa *line* yake ya utendaji anawajibika kwa TAMISEMI, kwa Serikali Kuu na kadhalika na hata kwa Halmashauri kwa maana hiyo

kwa zile Halmashauri kwa mfano kama za kwetu ambazo sisi kama Chama chenye Madiwani wengi tunaweza kumlazimisha akafanya kitu.

Kwa hiyo, ni lazima hawa wawe tofauti na wawajibike moja kwa moja kwa Tume na Tume iwasimamie kikamilifu hicho ndicho tunachokisema kama kifungu hiki kitasaidia kuleta amani na utulivu na kuwa na uchaguzi ulio wa haki na wa huru katika nchi yetu. Hiki kisiposimamiwa kitaendelea kuleta matatizo. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Rajab Kiravu pale anafahamu na namshukuru kwamba walichukua hatua. Kuna mahali ambapo tumefika na wenzangu ambao wanaona kwamba Upinzani unapoleta hizi kauli wanafikiri tunaleta kutoka hewani.

Naomba muelewe kwamba tunapoleta hizi kauli ni kutokana na uzoefu tulioupata kwenye maeneo yetu. Inawezekana huko kwenu hakuna matatizo, lakini sisi tuna matatizo makubwa unapofika Mkurugenzi anageuka anaacha kuwa msimamizi wa uchaguzi anaanza kuwa mtumishi wa Chama Tawala. Sasa hapo ndiyo tunaanza kuwa na matatizo. Lakini namshukuru Ndugu Rajab Kiravu pale pamoja na Jaji kwamba wamechukua hatua. Nadhani mahali pamoja ambapo tulipiga kelele ni kule Hai, ambapo Mkurugenzi ameondoka kabisa na timu ya Serikali anafuatana na kampeni timu ya Serikali na anakwenda kujibu maswali ya Serikali. Sasa je, akaenda na angefuatana na vyama vingine, je, angeweza kuachwa pale.

Nashukuru wamechukua hatua, nashukuru Serikali pia baada ya kelele hizo imemhamisha yule bwana. Kwa hiyo, hiki ndicho tunachosema wenzetu wasione tu Kambi Upinzani anasema kutoka hewani. Naomba tuelewane tunajenga nchi moja, nchi yenye heshima, nchi yenye amani, nchi yenye utulivu na wote tuna hisa katika kujenga utulivu huu na amani hii katika nchi hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, *independence* ya hawa watu isipohakikishwa tutaendelea kupiga kelele. Mimi sina tatizo akiendelea kuwa Mkurugenzi au hata angeendelea kuwa Katibu Tarafa, lakini tulipata tatizo. Mimi kule kwangu nilipata tatizo kubwa mwaka 2000 kwa sababu yule unayempelekea ambaye ni *public officer,* Katibu Kata, anakataa hata kupokea simu. Kiravu anakumbuka kwamba nilipaswa kupiga simu Dar es Salaam akaagizwa kutoka Dar es Salaam pokea fomu. Sasa tunapofikia hapa ni matatizo makubwa kabisa na ndiyo sababu inayoleta hii.

Kwa hiyo, tunachoomba ni tuhakikishe hawa watu kweli wanakuwa chini ya Tume na hawa watu kweli wanafanya kazi ya Tume ya Uchaguzi kwa lengo la kuleta uchaguzi sahihi, uchaguzi huru, uchaguzi ambao hauna ubaguzi kwa upande wowote ule. Uchaguzi lazima kuonekana kuwa huru ni lazima kweli uonekane kuwa huru siyo karatasi tu na sheria inaonyesha kwamba ni huru. Katika matendo ni lazima uchaguzi pia uonekane kwamba ni wa huru. *(Makofi)*

Kule kwa wenzetu katika *assessment* nyingi tulizofanya kwenye ngazi ya *SADC* chaguzi nyingi za Afrika zinaitwa kwamba ni za huru lakini siyo *fair.* Sasa Tanzania lazima tutoke hapa. Chaguzi zetu ni huru na hata tathmini iliyofanyika na kamati yetu

hata zile Tume zingine zilizoangalia uchaguzi wetu wa mwaka 2000 walisema uchaguzi wa Tanzania ulikuwa huru, hawana hakika sana na *fairness.* Kwa hiyo, tutoke kwenye hatua hiyo, twende sasa kuwa na uchaguzi huru na ambao pia ni *fair.*

Uchaguzi *fair* maana yake ni makando kando haya yote yaweze kurekebishwa, anayeweza kurekebisha ni moja tu ni Tume ya Uchaguzi. Iitwe huru, isiitwa huru mimi sina tatizo, *provided* zinasimamia ile misingi ya uchaguzi huru na wa haki.

Jambo lingine ambalo naomba nigusie kwa kifupi ni hili suala la vitambulisho. Ni kweli tusipoangalia tutapitisha hii sheria vifungu vyako hivi vinaonekana safi na takatifu. Lakini katika utendaji vifungu hivi haviwezi kuwa safi na takatifu kama vile vigezo na vile vitu vyote vinavyofanya vifungu vitekelezeke haviko *in place* moja ni kitambulisho.

Sasa hapa kwa kweli naomba bado Serikali bado itujibu, tulishaambiwa mara nyingi kwamba vitambulisho vya Taifa vinatengenezwa, *tender* ikatolewa ikaenda mahakamani, hatuna taarifa tene kulitokea kitu gani. Ile tender ni ya siku nyingi Sasa ikishatokea bado inafuata kitu gani? Je ni kweli kwamba lile suala bado mahakamani? Je ni kweli kwamba sasa baada ya mahakama kama imeisha tumeshindwa kuvitengeneza? Je, ni kweli na yule ambaye tulikuwa tumemlipa *advance* wakati ule kwa mabilioni ya hela je, mpaka sasa hivi zile hela zimekwenda wapi na kwa nini hili daftari leo lisipatikane? Mimi nafikiri Serikali ina swali la kujibu hapa. *(Makofi)*

Lakini vile vile mwaka jana tulipitisha katika Bajeti na mimi bahati nzuri niko katika Kamati husika, kuna fedha bilioni moja na laki nane kama sikosei zilizokuwa chini ya Kasma ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambazo nadhani sasa hivi zimehamishwa kwenda Tume. Je, sasa hivi, hivi vitambulisho vitapatikana au hapana?

Tukumbuke mwaka 2000 *harassment* iliyopatikana mipakani. Majimbo ya mipaka yanapata *harassment* kwa sababu hata uandikishaji ukifika Tume hii ya akina Kiravu ambayo ni watu wazuri watakatifu hawako tena kule chini, wanaoandikisha kule chini ni watu ambao wana maslahi mengine pia na hatujui wana maslahi ya aina gani.

Kwa hiyo, ili tuondoe ni lazima kwa kweli tuwe na vitambulisho ambavyo vitahakikisha kwamba hivi vifungu vya sheria iliyoko hapa vitatekelezeka vizuri. Ndiyo maana tunaongea kitu ambacho hakiko ndani ya vifungu ni kwa sababu vifungu kutekelezeka ni lazima makando kando ya vifungu yawepo.

Mimi nimeshiriki kwenye *observation mission,* nimepokea taarifa zote za *observation mission* na kama *SADC* tumekwishakupokea taarifa 10 sasa za nchi za Afrika hakuna nchi isipokuwa ni sisi ambao hatuna vitambulisho. Wengine wote wanaanza na vitambulisho na mimi nilishiriki, nchi kama Mozambique walikuwa vitani, nimekwenda Jimbo la Nampula, kilomita 200 ndani porini, watu wamekuwa na vitambulisho. Sasa nchi yetu ambayo toka juu mpaka nyumba 10 tunajua, hivi tumeshindwa nini kutengeneza vitambulisho?

Mheshimiwa Spika, hili kama Taifa ni lazima tupige kelele na tuhakikishe kwamba bado kuna mwaka mzima na nashukuru Tume sasa imeanza utaratibu hata wa kutengeneza vitambulisho na kuandikisha wapiga kura kwa Kanda. Mimi naomba uandaliwe utaratibu wa kupata vitambulisho na iendane sambamba na hili Serikali itujibu leo vitambulisho hivi vitapatikana lini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kugusia kifungu cha 26(4) ambacho mimi kinanipa kidogo pia wasi wasi. Kifungu hiki kinazungumzia *The Commission shall, on the election the day, upon the occurrance of an event that prevents an election to take place, appoint another day of election.* Kifungu kilivyokaa hakina tatizo kwamba ikitokea vurugu kwa sababu fulani Tume inaweza ikaamua kuahirisha uchaguzi wa Jimbo hilo au majimbo hayo mpaka siku nyingine.

Naomba kutoa tahadhari, kifungu hiki kisipoangaliwa Mheshimiwa Spika, kitatumika vibaya. Tatizo haliko kwenye maneno, tatizo ni *criteria* haziko wazi. Unapofika mahali unataka kuahirisha Uchaguzi ni lazima kuwe na *criteria objective* zinaonekana na kila mmoja na wote tukakubaliana. Mimi nafahamu mwaka 1999 kwangu pale hiyo siyo ya Tume lakini ilikuwa ni ya Serikali za Mitaa, walienda wakaahirisha uchaguzi wakatangaza, uchaguzi utatangazwa siku nyingine. Anaenda kutangaza Mkurugenzi.

Usiku wakapitisha lori wakaenda kutoa taarifa na kukusanya watu asubuhi, asubuhi ukafanyika uchaguzi wa Serikali. Tumelalamika mpaka kwa Waziri husika, hakuna hatua iliyotokea. Anayehusika ni yule yule Mkurugenzi huyo huyo ndiye aliyekwenda kuahirisha. Mkurugenzi huyo huyo asubuhi anafanya uchaguzi na mimi nikanyang'anywa Mwenyekiti wa Kijiji.

Kwa hiyo, tunachosema ni Tume ikipitisha Sheria ya namna hii, ni lazima wale wote walio chini yake katika ngazi zote iwasimamie na wanakuja kutoa taarifa maana yake Ndugu Kiravu amekaa Dar es Salaam hajui kule Rukwa, vurugu imetokea imesabishwa na nini. Inawezekana watu wameona tu kwamba wanashindwa uchaguzi kundi la watu 20, 30 wakafanya fujo na kwa kuwa wanafanya fujo kwa hiyo uchaguzi uahirishwe, wanapeleka kwa Kiravu, wanakubali au Jaji Makame.

Kwa hiyo, mimi ninachoomba *criteria* hizi ziwe *objective.* Tume itengeneze mwongozo kamili ambao utapelekwa mpaka chini na hii naungana na alichosema Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga kwamba ni lazima kuwe na *Party Liaison Committee* ili katika mazingira ya namna hiyo sasa kuwe na uwezekano na hii si lazima iwe kwenye Sheria, inaweza kuwa kwenye *regulation.*

Kwa hiyo, tunaomba tu, mtakapotengeneza miongozo yenu mhakikishe kwamba kuna *Party Liaison Committee* ili hata tukio la namna hii linapotokea ijadiliwe na vyama vyote kuondoa *misunderstanding* na wenzetu kwa mfano Malawi walikuwa nayo na wenzetu *South Africa* walikuwa nayo. Sababu ya kuondoa na kuwa na amani na utulivu katika ngazi zote ni kwa sababu kulikuwa na mashirikiano na mawasiliano katika ngazi zote tangu Taifa mpaka kwenye Wilaya mpaka kwenye ngazi ya *Ward* ambapo yule wa chini anapigiwa kura.

Kwa hiyo, nadhani tukiwa na hali hii hata kifungu hiki hakitatumika vibaya, mimi vinginevyo kifungu hiki sina tatizo. Ninachoomba ni utakatifu tu wa watu wote wanaosimamia hivi vifungu waweze kuvisimamia ili pale inapotokea sababu nzito ya kutaka uchaguzi uahirishwe sababu hizo zikubalike angalau na kundi la watu isiwe ni mtu mmoja, isiwe ikawa ni Mkurugenzi peke yake akakaa chini kwa sababu amesukumwa na watu fulani akasema naomba Mkurugenzi aahirishe uchaguzi katika jimbo hili au katika Kata hii.

Hii naomba sana Mheshimiwa Spika, liangaliwe vinginevyo tutajenga na kuondoa heshima ya Taifa ambayo kwa kweli tumejijengea. Kuhusu hili la wenzetu walioko nje, naomba niliseme tena kwa sababu ni juzi tu tumerudi na wenzangu kutoka *SADC.* Mmetutuma ninyi wenyewe, tumekaa pale Namibia na naomba nitoe mfano wa Namibia pekee ambapo kuna kaya zaidi ya 50 na katika kaya zaidi ya 50 tuna wapiga wanaokaribia 100 na kitu. Mia moja na kitu ni sawa na kijiji. Katika vijiji vyetu vidogo.

Sasa hawa tunapowanyima haki ya kupiga kura na hawa wengi wao ni watu wetu tumewatuma, ukiondoa wale wachache wameenda kwa biashara, wale *pay day,* lakini wengi ni watu tumewatuma. Wanafanya kazi za Serikali na ni watu wetu ambao wanafuatilia kwa karibu sana maslahi ya Taifa lao. Kwa hiyo, kwa kweli wangependa.

Mimi naomba katika *schedule of amendment* itakayoletwa na Waziri kabla ya kuahirisha, angalau uwezekano wa watu hawa uangaliwe hata kama utaratibu haukuandaliwa sasa bado tuna mwaka mzima ili *mechanism* ya hawa kuwawezesha wapige kura iweze kuandaliwa na kama kuna ulazima wa sheria basi bado tuna muda wa kutosha wa kuleta hiyo.

Lakini ile *principal* angalau iweze kukubalika. Tuna watu wengi, hiyo ni nchi moja, kuna zaidi ya watu 100 wanataka kupiga kura na walikuja wao na uongozi wao pale Namibia. Wamekuja wakatuambia Watanzania sisi tunafuatilia mambo kwa karibu. Tunaomba sasa hatima yetu mtuambie. Sasa mimi nafikiri ni bahati mbaya kwamba hatujapita nchi nyingi lakini kilio hiki kinaelezwa na wenzetu kila mahali.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hii. Awali ya yote kabisa napenda kupongeza Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, aliyewasilisha Muswada huu kwa kuleta Muswada huu ambao una shabaha ya kuongeza ufanisi katika chaguzi mbalimbali, uchaguzi mkuu pamoja na chaguzi za Serikali za Mitaa. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Ila nina machache tu ya kugusia. Ninakubaliana kabisa kwamba daftari la wapiga kura ni muhimu na tumechelewa. Kwa hiyo, tusizidi kuchelewa tena. Tunalihitaji ili litumike katika uchaguzi wa mwaka ujao na ni muhimu. Pengine wakati wa chama kimoja isingekuwa kitu cha kipaumbele, lakini kwa sasa hivi kwenye uchaguzi unahusisha vyama vingi, sasa hivi nadhani vinafikia 16 vilivyoandikishwa. Ni vizuri

tukawa na uhakika wa watu ambao watakuwa wamefikia umri wa kupiga kura na wanastahili kupiga kura.

Kwa hiyo, Daftari la Wapigakura kwa kweli siyo kitu tena cha kuzungumzia kwamba kiwepo au kisiwepo, ni lazima kiwepo. Kwa hiyo, mimi naunga mkono Daftari hilo lishughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uandikishaji wa wapiga kura. Mimi nakubaliana na Serikali kwamba tutumie vyombo vilivyopo. Kuanza kuunda vyombo vingine wakati tunavyo vingine vilivyopo ambavyo visipotumika kutumika vizuri zaidi ni kupoteza muda na mimi nashauri kwamba watumike Waandikishaji na Waandikishaji Wasaidizi ambao wana ajira za kudumu na ambao hata Sheria zinaweza kuwabana kama watakwenda kinyume na taratibu za kazi.

Kwa hiyo, huwezi kuepuka Maofisa wa Serikali za Mitaa ndiyo walioko kule kwenye watu wengi. Sasa kuanzisha Kada nyingine hizi kwa kweli tutakwenda kinyume kabisa na hizi *reform* za Serikali ambazo tunazifanya kwamba kuwe na watu wachache lakini wenye utaalam mbalimbali. Na hapa ningependa kupendekeza kwamba suala la mafunzo liende na zoezi hili kwamba yaandaliwe mafunzo rasmi kabisa ya uandikishaji wa wapiga kura na mafunzo hayo yaingizwe vilevile nafasi ya kuona sehemu ambako daftari linatumika na kujua matatizo waliyopata na mafanikio waliyoyapata. Ni muhimu kabisa kutoa mafunzo.

Kwa hiyo, mafunzo yataondoa hata dosari ambazo zinadokezwa hapa, kwamba pengine wengine ni wa CCM. Lakini kama mtu ni *professional* anajua taratibu za kushughulikia kitu fulani, basi hata uwajibikaji wake unakwenda kwa mtu yule ambaye anasimamia kitu hicho na sasa hivi mimi nashangaa kwa nini suala hili lisisimamiwe na Halmashauri za Wilaya ikiwa hata *technical functions* ziko kule. Madaktari kule Wilayani wanasimamiwa na Halmashauri za Wilaya, sembuse waandikishaji wa wapiga kura.

Mimi nadhani kutakuwa na miiko na maadili ya kushughulikia zoezi hili. Huko Wilayani wako watu wazuri tu tena waaminifu tu. Kwa hiyo, tusianze kuwahukumu kabla ya kuona makosa ambayo yatajitokeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitambulisho, mimi nadhani tuzungumzie vitambulisho vinavyohusiana na kuandikisha Wapiga kura. Vitambulisho vya Uraia vina Sheria yake ya Uraia ya Uhamiaji, kwa hiyo, kuvichomeka hapa ni kwenda kinyume cha taratibu na vitambulisho hivyo vya Uraia haitoi jibu la upigaji kura bila kuwa na Daftari la Wapiga kura.

Tunazungumzia sheria ya uchaguzi na vitambulisho vya uchaguzi ni *specific.* Sasa hivi, vitambulisho vya Uraia ni muhimu, lakini katika sheria hii siyo mahali pake. Kwa hiyo, napenda kutoa ushauri kwamba kama kuna mtu ana hoja binafsi kwa nini asiilete tuizungumzie kwa maana ya sheria ya Uraia na Uhamiaji. Hata mimi naona kuna umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kwamba vitambulisho vinavyotengenezwa vitengenezwe kwa kuzingatia mazingira ya utunzaji. Kitambulisho kinachokwenda Mgwashi.

Nashukuru sana Kamati ya Bunge ya Sheria, Katiba na Utawala, imetembelea eneo langu moja linaloitwa Mgwashi. Sasa utengeneze kitambulisho cha Mgwashi. Angalia mazingira ya Mgwashi na utunzaji wa kitambulisho hicho kwa maana kwamba kitanyeshewa na mvua, kitapata moshi na kadahalika. Sasa uzingatie hayo kwamba kiwe ni kitambulisho ambacho kinahimili mazingira ya namna hiyo na ningeshauri wanaokitengeneza kiwe na sehemu ya kuwekea hata kamba, kitundu cha kuwekea kamba ili mtu aweze kukivaa kwenye shingo au mahali pengine. Huu ni ushauri wa kufanya kitambulisho hicho kisipotee haraka haraka.

Vile vile kuwe na utaratibu wa kutoa taarifa, kama kimepotea. Taarifa itolewe kwenye Serikali iliyopo karibu kama ni kwenye Kitongoji, kuna Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji, kama ni kwenye Kijiji basi kuna Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji. I tolewe taarifa kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji na yeye aiandikie barua kuarifu. Ule ndiyo udhibiti wa vitambulisho na hata vitambulisho tulivyonavyo Wabunge tulivyopewa hapa, tumepewa na Mheshimiwa Spika, vinasema kikipotea toa taarifa.

Kwa hiyo, navyo vitolewe taarifa visiwe kama ni karatasi tu ambayo inaweza kupotea na ndiyo maana nadhani Serikali imezungumzia kitambulisho ambao ni tofauti na shahada ambayo ni karatasi tu na inaweza ikawekwa mahali popote, ikapotea au hata ikapasuka au ikachakaa haraka.

Mheshimiwa Spika, suala hili lifuatane na elimu ya kudumu ya uraia ambayo itazungumzia suala la vitambulisho vya kupigia kura. Kwa hiyo, isiwe ni kitu cha kupita tu na kuwakumbusha wananchi kwamba kitambulisho chako cha kupigia kura kimepotea, piga ripoti haraka sana kimepotelea wapi ili uweze kufanyiwa utaratibu wa kupata kitambulisho kingine. Kisiwe ni kitambulisho tena cha kuingiza katika mlolongo wa kupata huduma na rushwa ikaingia hapo tena. Vitambulisho hivyo kwa kweli viwe na udhibit mzuri sana visije vikaingizwa kwenye mlolongo wa huduma ambao umezungukwa na mazingira ya kutoa chochote ili uweze kupewa kitambulisho cha kupigia kura.

Mheshimiwa Spika, mimi Serikali imenifurahisha sana kuweka tamko la Wagombea Urais kuhusu sifa zao. Hii ni hatua nzuri sana. Tuna watu hapa wamejipa madigrii, wamejipa mashahada chungu nzima. Hatuna uhakika na huwezi kumwuliza hii umeipata wapi, unamwonea. Lakini ikifika kugombea urais kwa kweli watoe tamko mbele ya Jaji na vile vile zile shahada na vyeti viandikishwe (*registration of certificates and professional documents)* ili kama atatamka uongo na huku amezi-*register* maana yake ni *forgery.* Kwa sababu huulizwi hapa. Hapana budi tuulizane wewe shahada umeipata wapi? Mtu anasema mimi ni *Doctor,* basi tukubali tu?

Hata mimi hapa naweza kusema leo ni *Doctor* unaniulizia nini mbona wengine hukuwauliza. Lakini ni vizuri katika Bunge hili kama mtu amepata Shahada na vyeti

vyake vizuri basi vyote alivitoa kwa Spika, akamwambia ni hivi. Tufike mahali kwa kweli tuzungumzie vitu ambavyo havina utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziko shahada wanazopewa watu za heshima, zinajulikana wala hazina matatizo, lakini tuwe na uhakika ni chuo gani kimempa ili umpe heshima ambayo inastahili. Kwa sababu kuna uwezekano hapa kwa kutumia haya madudu haya tuweze kumtuma mtu mahali unadhani ni *material,* mkapata adha kubwa sana ya kuuliza na kuchafulia watu wengine ambao wamepata shahada na vyeti vizuri. Mimi simzungumzi mtu yeyote, lakini natoa *comments* ambazo naziona zina mantiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani kwenye Urais tuanzie hapo halafu tuje kwa Wabunge nao.

Napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na napenda kutamka kwamba naunga mkono Muswada huu wa Sheria wa Kurekebisha Sheria ya Uchaguzi hapa nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu na mimi nichangie.

Kama kawaida Mheshimiwa Danhi Makanga, asije akanilaumu kwamba sikumpongeza. Nampongeza kwa ushindi wake na nawapongeza wananchi wa Bariadi kwa sababu sidhani kama Mheshimiwa Makanga alishinda kwa sababu ya CCM, kwa sababu hata alipokuwa UDP alikuwa anashinda. Kwa hiyo, nawapongeza waliompigia kura kwamba wana imani naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli hata mimi naunga mkono Muswada huu ili kuupitisha na kuhakikisha kwamba daftari la wapiga kura linakamilishwa haraka iwezekanavyo na uchaguzi unakwenda vizuri. Sasa bahati mbaya mjukuu wangu Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, ameshaondoka, nilitaka kumhakikishia kwamba mimi siyo CCM na Serikali siitetei lakini sina uhakika kama Serikali imeshinikizwa na mtu kutoka nje. Kwa sababu hii iko kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba liwepo Daftari la Wapiga kura. Kwa hiyo, haliko huko mjukuu wangu Mahanga aelewe hilo.

Sasa nilikuwa nataka kuchangia katika *Section 4(c)* ambayo wanawapa Tume madaraka ya kudhibiti na kutoa elimu kwa wapiga kura. Hakuna sheria nyingine inayotoa mamlaka kwa chombo kingine. Lakini kwa *experience* kulikuwa na Taasisi na asasi mbalimbali ambazo zilikuwa zikitoa elimu ya uraia. Sasa sijui katika vipengele na Bajeti za Idara zilizoko pale Tume ya Uchaguzi kwamba kuna watu maalum ambao watasambaa nchi nzima wameshaandaa *material* ya kuwaelimisha watu elimu ya kupiga kura.

Lakini tunavyojua watu kama *TEMCO* na Mashirika mengine walikuwa wakifanya kazi hiyo kuwaelimisha wapiga kura. Sasa hii ya kutaka kudhibiti sijui inatoka wapi. Maana yake wamepewa wao peke yao na huenda *resources* zisitoshe na kwa hiyo sijui inakuwaje.

Kwa hiyo, tunataka kuweka angalizo hapa kwamba wasije wakahodhi bila ya kazi yenyewe kufanyika. Kwa sababu tunachotaka pamoja na kuhodhi lakini lazima kazi ile ifanyike. Sasa katika soko huria na kila kitu huria kuhodhi si vizuri.

Mheshimiwa Spika, liko hili lingine kifungu cha 7(a) kuhusu kuwateua Wakurugenzi wa Miji, Wakurugenzi wa Wilaya kuwa ndiyo waandikishaji na bila shaka katika mazingira ya utamaduni wetu ndiyo hawa hawa watakuwa ndiyo wasimamizi.

Mheshimiwa Spika, kuna mawazo ambayo yanakinzana kwamba hawa ndiyo wasimamie au ndiyo waandikishe na wengine kuwa Kambi ya Upinzani wanakuwa na wasiwasi kwamba wakiandikisha na wakati mwingine kusimamia haki haiwezi kutendekeza na wengine wakasifia kwamba ni busara kwa Serikali kusema wao ndiyo wasimamie.

Sasa busara ni busara na inategemea kila mmoja maslahi yake yalipo ndiko huona busara. Naona kama mimi siamini kuwepo kwa Mungu naamini kuwepo kwa shetani basi maslahi yangu yananituma nihakikishe kwamba hii busara ya shetani ndiyo inayotawala na wale wanaoamini kwa Mungu basi wanaona basi busara ile ya Mungu ndiyo nzuri. Lakini la msingi nililotaka kusema hapa ni kwamba tunaposema Tume Huru, pale ngazi ya Kitaifa pale hatuna matatizo sana. Sasa tunaposema kule Wilayani tuanzishe watu wengine wanasema unajua hela, unajua hela. Hili la hela sijui kwamba linasemwa sasa. Hata wakati wa kuanzisha *proposal* ya kuanzisha mfumo wa vyama vingi, watu walipiga kelele kuhusu suala la hela.

Hivi nilikuwa najiuliza, tuna Polisi hapa, tuna Sheria za kuzuia Rushwa, kila raia achukie rushwa. Kuna watu wa Usalama wa Taifa, lakini hiyo, haikuizuia Serikali kuanzisha *PCB* na siyo kuianzisha ikaiweka Dar es Salaam inaipeleka mpaka Wilayani. Sasa hivi wanatumia mabilioni ya pesa kama bilioni 30. Sasa katika hilo, hapa hapana. Mbona hatusemi Afisa Usalama pale yeye anafanya nini. Kwani yeye hakamati wanaokula rushwa? Kwa nini hatusemi *OCD* naye asiwakamate, mwingine naye anachukua. Lakini kwa hilo tumeona siyo kupoteza hela, tumewaweka. Japo hawajamkamata hata kigogo mmoja.

Sasa hiyo haimo humu kwenye Muswada, lakini tunakuwa na wasiwasi kwamba Wakurugenzi wameajiriwa na Ofisi ya Rais na wana mhimili Mkuu wa Wilaya ni mhimili pale na wana mhimili. Sasa wasi wasi huu unatokana na maagizo. Mtu amekuja hapa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania anatuambia hapa alikuwa anasikitishwa kwa kweli na udhaifu wa vyama vya upinzani na mantiki yake ni udhaifu ule kwamba tuko wachache humu ndani.

Busara na hekima ya hali ya juu na walishaiona watu wa Kyerwa ndiyo wakanileta hapa. Lakini sasa inapotokea mtu mwingine anaamrisha kwamba wewe *DC* kama kwenye jimbo hilo wanashindwa utoe. Sasa *DC* yeye siye Mbunge aliyepo, wala *DC* yeye siyo Katibu wa Chama wala siyo Mwenyekiti wa Chama na *DC* mnamwonea, maana yake ni kutaka ku-*temper* na *process* nzima na kwa kweli *this is pollution of democracy.*

Mheshimiwa Spika, sisi tulitegemea kwamba watu wa namna hiyo wanapokwenda kinyume na busara ya Rais wangekamatwa halafu wanashughulikiwa. Sasa siyo hivyo, lakini tuache watu wafanye kazi yao. Maana yake mimi ninachosema ni uzoefu, nimekwenda kwenye jimbo langu nikakuta *DC* aliyekuwepo amekwenda pale amejipeleka na viongozi wa CCM wale ni kazi yao. Katibu wa CCM akasema Mutungirehi, hafanyi kazi. Lakini sidhani kama hii kazi ya *DC* kwenda anamtuma Mutungirehi hafai. Hivi mimi nikija hapa nikaanza kusema *DC* fulani amefanya hivi, nadhani hiyo siyo kuheshimiana.

Sasa tunadhani hii tunapoitana sisi, ndiyo huu wasiwasi wetu kwamba watafika mahala watu wengine wanawaambia hebu kafanye kazi hii. Lakini sisi tunachosema kama ile Tume tumemwajiri mtu pale ameajiriwa afanye kazi ya *registration* kwa sababu bahati nzuri wameshapata kazi ya kuandikisha watu kila mwaka kwa ajili ya daftari hilo, asimamie uchaguzi, Ofisi yake inakuwepo. Anakuwa pale kama alivyo Hakimu wa Mahakama ya Wilaya. Hawezi kuamrishwa na Mkuu wa Mkoa wala mtu mwingine kwamba hukumu hivi usipohukumu utanitambua. Usalama wake umelindwa. Lakini huyu kwa njia moja au nyingine mnaweza kujidanganya kwamba tutamlinda linda, lakini sasa kuna mtu amemwajiri. Onyo wakisema kwamba mtanitambua, ndiyo kitu ambacho tunajaribu kukwepa katika hilo.

Mheshimiwa Spika, ninajua hamtakubaliana na mimi na kipengele hiki kitapita hivyo. Sasa inabidi tuweke kipengele hapa sasa kwamba kama mtu amekwisha kuaminiwa na amekula kiapo na bado akashinikishwa basi kiwekwe kipengele hapa kwamba watakapotangaza, watakaosimamia awe ni Mkurugenzi wa Mji au Halmashauri, basi kama kuna watu hawaridhiki naye wamwekee pingamizi tuweke hapa. Aweke pingamizi kwamba mtu huyo hatukubaliani na Tume ichunguze ikijiridhisha imtoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipo kipengele cha kusema Rais na Makamu wake wakati wanagombea waende mbele ya Jaji. Sawa! Lakini mimi napata wasiwasi kwamba waende halafu iweje. Kuna maana mbili pale, waende kama yeye anatoa taarifa za kufoji, anasema ana *PhD* au ana cheti hiki. Labda pengine aweze kuwekewa pingamizi katika hatua za awali.

Lakini atakapokuja katika hatua ambapo bado mnaendelea kumfuatilia huyu ambaye alidanganya na akapitishwa pale, baada ya uchaguzi hamuwezi kumwadhibu kwa sababu mtakuwa mnavunja Katiba ya nchi. Katiba ya nchi kifungu cha 41 nadhani kifungu kidogo cha 5, kinasema Tume imeshamtangaza aliiba kura au alifoji cheki au alifanyaje au siyo raia, hakuna chombo wala mamlaka wala Mahakama itakayomjadili.

Mheshimiwa Spika, sasa kama hivyo, ndivyo ilivyo hata hii mimi nashindwa kujua mantiki yake ukiacha. Lakini kama itahidi kwamba pamoja na mashtaka ambayo yalipaswa kuwepo na kudhibitiwa kwa sababu alidanganya, kipengele hiki kingelikuwa na uzito unaostahili. Sasa *unless* tukubaliane kwamba tukiangalie na kile kingine kilichoko kwenye Katiba kwamba tutakapokuja kubadilisha Katiba kile tukifute.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na kipengele hapa ambacho kimeipa Tume kwamba wao waamue muda wa kuandika daftari la wapiga kura. Sisi kama Bunge tupitishe sheria wala hatuweki muda kwamba wao watakapokuwa wanaandikisha wafanye kazi hiyo kwa muda wa miezi mingapi, hamna.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nashindwa kuelewa maana yake nimekaa hapa Bungeni kila tunapotunga sheria huwa tunaweka muda. Wewe fulani unashughulikia rufaa muda fulani. Wewe fulani unashughulikia hii muda fulani na hiyo inakupa nafasi kwamba wewe hukutimiza hiyo kwa muda ule uliopangwa na siyo mtu akulalamikie kwamba wewe madhumuni yako ya kutimiza kwa muda uliopangwa kisheria unataka kuharibu hii, anakushtaki.

Sasa muda haupo, wameandika wanavyotaka, hata wakitaka kuandika mpaka siku ya tarehe labda ya tarehe 30 Oktoba, 2005 wanaweka. Mimi nadhani ni bora tuwe tunaweka kikomo kwamba ifikapo wawe wamejitahidi na hiyo itakusaidia hata wao Tume kupewa hela na nyenzo ambazo tulikubaliana. Lakini kama tukiacha hivi kila unayekwenda kumwomba hela na yeye kama ana mambo yake atakuambia subiri. Kwa hiyo, tulitaka tuliseme hilo na tulisisitizie kwamba ni mambo ambayo ni ya msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo na *actually* yale mengine hawatayakubali, lakini tumeongeza huyu anayeteuliwa huyu awekewe pingamizi kama ni mtu wa ajabu ajabu. Maana yake nilikuwa naulizwa na hili silisemi kwamba lazima atakuwa anawaonea watu wa upinzani pengine anaweza kuwa na ugomvi wake tu na mtu wa CCM kwa hiyo, mtu yeyote tu anaweza kuwa pale ana ugomvi anataka kuonea, unamwekea pingamizi.

Kwa hiyo, mambo kama yanaenda hivyo inakuwa vizuri na wakati unafanya hili, tukubaliane nadhani Serikali itatoa kauli kwamba sheria tumeshazitunga kwa sababu hamtabadilisha ni watumishi wa Serikali. Mtu yeyote anayewaamrisha kama kuna ushahidi wa barua au wa kusema kwenye mikutano ya hadhara anawaamrisha watendaji, akamatwe afungwe miaka 40 na viboko viwili. Ahsante. *(Kicheko)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya mwisho na mimi kuchangia angalau machache katika Muswada huu wa Sheria ya Kurekebisha ya Uchaguzi ya mwaka 2004 *(Electoral Miscellaneous Amendment)*.

Sheria hii ni viashiria tu vya malalamiko na matukio mbalimbali na mapungufu yaliyojitokeza katika ushauri wa Wabunge katika Sheria Na. 1, 1985 na Sheria Na. 4 ya mwaka 1979. Katikati kulifanyika marekebisho mengi ambayo sitaki kuyataja sasa ilitokea hili la daftari la wapiga kura. Huku ni kujiwekea taratibu mzuri ili kujua ni nani, yuko wapi na anafanya nini.

Ilitokea kwamba mtu alijiandikisha mara tatu, mara nne, mara tano kwa sababu zile hati za kupigia kura zilikuwa hazina picha. Sasa hii nashukuru sana itakuwa na picha. Kwa hiyo, mtu hawezi akajibadilisha sura, kama ile picha iliyotoka juzi kwenye gazeti, mtu mmoja ana sura 12. Sasa kwa hii haiwezekani, kwa sababu atakuwa na picha

yake ile ile. Kwa hiyo, mtu atapiga kura pale pale alipoandikishwa na atakuwa mtu yule yule kwa maeneo hayo hayo.

Kwa hiyo, nadhani huu ni utaratibu mzuri tu. Nilikuwa namwuliza Katibu wa Tume pale, kwamba kuna majimbo mangapi? Kwa bahati mzuri kumbe kwa utaratibu wa Kamisheni yako umetukatia tayari eneo kwamba tuna majimbo ya uchaguzi karibuni 231 katika nchi hii naye nikamwambia je, una *staff* wangapi katika Tume ya Uchaguzi ambao watakidhi katika kusimamia majimbo hayo?

Nadhani wako wachache sana, hakuweza hata kunijibu, kusudi waweze kuwapanga wafanye kazi ya Tume kama inavyoshauriwa na baadhi ya Wabunge. Jambo ambalo haliwezekani. Kwa sababu Tume ina ratibu na kusimamia lakini katika maeneo mengine hutoa majukumu mengine.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo Tume inaweza ikayafanya kama Tume, lakini maeneo mengine unaweza ukatuma kitu kufanya kitu hicho, mvua ingekuwa inanyesha mahali pale pale inapotegemewa.

Lakini kwa sababu mawingu hutumwa na upepo, basi wakati mwingine na upepo unaweza ukategemea madaraka kupeleka mvua maeneo mengine kwa utaratibu huu ambao Tume inafanya kwa kutumia vyombo vingine vilivyopo. Kwa kutegemea ulichonacho, usitegemee unachokitafuta kwa gharama nyingine.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni kuwatwisha mzigo Watanzania kwa gharama zisizowezekana.

Mheshimiwa Spika, naanza na kipengele namba (c) cha sheria hii ambayo tunarekebisha *Clause Na.7 to 15* amesema tuandike *as 8 to 16,* sawa. Sasa ukija kwenye *renumbering* hapa chini wanasema kuna *Section (G)* inasema kwamba *Clause No.16* inakuwa *renumbering as follows,* unaweka 17 pale. Namba (H) wanasema sasa una-*delete 19.*

Halafu *Section (I)* inasema *the numbering Clause 16 - 33* inakuwa *18 to 34* pale kuna namba moja ina-*miss* nataka nipate maelezo kidogo kama kweli kwa mahesabu yangu au labda nimekosea, kuna moja ina *miss* pale ukiitoa hiyo. Hapo kuna *renumbering* ya *35 to 36* kuna namba moja imeongezeka kwa sababu 34 inakuwa *added* pale juu kwenye kipengele namba (J).

Baada ya kusema mahesabu hayo kwa kuwa hatufanyi mahesabu katika *tuition* naingia kwenye Muswada wenyewe wa sheria. Kwa kweli mengi yalizungumzwa kuhusu Daftari la Wapiga Kura na tulilingoja kwa hamu sana. Demokrasia ina gharama lakini haina vipuri walioharibu demokrasia duniani wameleta vurugu baridi, kashfa za kina na maisha ya kutegeana katika nchi zao. Kwa hiyo, demokrasia kwa misingi yoyote Serikali iliyo makini inatumia Katiba na Sheria mara nyingi huangalia taratibu zinazoendeshwa katika nchi yake ili kuona kama yapo mapungufu kuyaziba na sio kuyaziba kwa mpigo bali huyaziba kwa taratibu ambazo zinatokana na uwezo na taratibu ambazo

zinazowezekana ili kuweza kuendesha nchi hiyo katika taratibu nzuri kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, demokrasia inaanzia kwa wapiga kura wenyewe tukianza kuwazungumzia wapiga kura, kuwaainisha, kuwaratibu na kuwaandikisha katika maeneo yao, hapo wapigiwa kura malalamiko na manung'uniko yatapungua. Ingawa Kwame Nkhurumah alionya kwenye kitabu kinachoitwa: *"Pan Africanism"*. Toleo la mwaka 1970 ukurasa wa 105. Akasema ingawaje demokrasia inafahamika kwa baadhi ya wanasiasa, *I quote,* akasema: *"Even though persuading while they are reconstructing a various nation state, African leaders including ourselves we are still using the term of democracy to describe our respective effort then upon the need of democracy published.* Kwa hiyo, tunaeleza juhudi zinazofanywa katika maendeleo yetu ndio maana ya demokrasia. Demokrasia ina maana pana kweli kweli. Watu wengi hutaja mahali wanapopasikitikia huona sio demokrasia mahali panapovutia husema demokrasia zote ni demokrasia zenye mapungufu na demokrasia ambazo zinakwenda na uwiano mzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo basi, tumetoa madaraka kwa Tume pamoja na kwamba wanasema sio Tume huru lakini mimi nasema Tume imara tunaiimarisha kwa sababu Tume huru mara nyingi sio Tume ambayo inatoka mbinguni ikatua lazima iundwe na vyombo vilivyopo madarakani kwa mujibu wa Katiba. Sasa uhuru wa kufanya mambo yake katika kutoa maamuzi kama kuleta sheria za marekebisho mbalimbali, usimamizi, kuratibu na kutoa madaraka kwa watu wanaohusika huo ndio uhuru wa Tume katika kushughulikia maeneo ambayo yanayomhusu. Naomba muendelee kwa taarifa hiyo.

Nimeshukuru tu *from the horse's mouth,* Ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Slaa, ambaye ni mmoja wa viongozi wakubwa sana wa Vyama vya Upinzani hapa nchini amekiri kwamba Tume inafanya kazi nzuri. Natoa pongezi kweli kweli kwa sababu nilikuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, siku moja wakati ulipokuwa unahojiwa kwa kuulizwa maswali katika kipindi kile cha: "Tuambie", ulikuwa unatoa maana ya uhuru wa vyombo vilivyopo na ukaitaja Tume madhubuti, Tume huru. Nilisikitika siku moja nilipoangalia tena *TV* nikaona baadhi ya viongozi wakiisusia wakatoka. Nadhani sasa yameisha mtakapoitwa tena mtaenda kuzungumzia masuala haya. Raia wenye kukataa haki yao kwa kweli ni wale ambao hawana hakika kwamba wataongozwa na nani na kwa utaratibu gani, sasa natoa wito daftari linakuja jiandikisheni.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuandikisha kwa mfano kuna vyuo ambavyo vina wanafunzi zaidi ya 2000, 3000 ambao wataandikishwa mahali walipo kwa ajili ya kupiga kura pale walipo kuna wakati watapata likizo au watamaliza masomo yao na ni wakati wa kupiga kura, itakuwaje? Naomba hiyo iwekwe bayana kwa ajili ya kuepuka mtu kupiga kura pale pale, maeneo yale yale, mtu yule yule au kutakuwa na uhamisho wa mtu kwenda kupigia kura kwingine?

Mheshimiwa Spika, kwa viwanda vya msimu kwa mfano Mtibwa na Kilombero wakati wa kupiga kura viwanda hivyo vinafungwa wanarudi nyumbani mfano Zanzibar na maeneo mengine, sasa nao ielezwe itakuwaje.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile wasimamizi wale ambao wanakwenda kusimamia zoezi la upigaji kura nao ni wapiga kura vile vile sio wasimamizi tu wanataka wapate viongozi, watapigia kura maeneo gani?

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna masuala ya wagombea wanaopenda kujitoa waelezwe mapema tu kwamba mgombea kwa nini ujaze fomu halafu ujitoe? Wasishawishiwe wajiangalie kama kweli wana ubavu wa kuingia katika mapambano. Kama huna ubavu basi usipende kupoteza fedha za watu kuchapisha picha yako halafu unasema mimi najitoa.

Kwa kweli mapema kama kuna mtu anakushawishi mwambie bwana usiniweke kwenye matata. Usijiingize kwenye Jimbo ambalo kwa kweli watu wamejizatiti pale na Chama kipo imara halafu baadaye unasema unajitoa kwa kweli itabiti ulipe gharama. Kwa nini usiache tu watu wakapita bila kupingwa katika maeneo hayo mkaweka watu katika maeneo ambayo mnategemea? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine nimeona masanduku ya kupigia kura ni *transparency* kweli lakini wakati fulani nilipendekeza watu walicheka hapa nilisema hivi kwa nini kila Chama kisiwe na sanduku lake ili kama hakuna karatasi aondoke mapema kabisa. Kwa sababu anashuhudia kwenye sanduku lake hakuna karatasi hakuna haja ya kung'ang'ania pale anaondoka anaona yanajaa kwenye sanduku lingine kwa hiyo unajiondokea mapema kwa sababu wakati wa kuhesabu wakitoa matokeo huwa baadhi ya watu wanafanya vurugu sana.

Kwa hiyo, ningeomba waondoke mapema baada ya kuona sanduku la Chama chake hakuna kitu. Ningependekeza kila sanduku libandikwe jina la Chama fulani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine Tume ya Uchaguzi, hii ni chagizo na changamoto ambayo imepewa kwa hiyo basi madaraka mliyopewa ni makubwa yalingane na ridhaa ya Watanzania. Mpo kwa mujibu wa sheria mtumie vitengo na vyombo mlivyokabidhiwa kama ni sehemu yenu ya utekelezaji wa demokrasia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja kwa sababu inalenga kufanya uchaguzi kufanyika kwa ufanisi, uwazi na kuondoa malalamiko yasiyo ya lazima. Pamoja na hayo nina machache ya kushauri. Katika Kifungu cha 4C, kuhusu elimu kwa wapiga kura ili wapiga kura wote wapate elimu nashauri:-

(i) Itolewe kimaeneo kama Kata au Vijiji.

(ii) Kutokana na maeneo kutofautiana kihali ya hewa na mazingira, watoa elimu wawe wengi na ikiwezekana watoke katika maeneo waliyoyazoea. Mtoa elimu mgeni na eneo husika anaweza kuathirika kihali ya hewa au kimazoea.

(iii) Kabla ya kuanza kutolewa elimu hiyo wananchi watangaziwe juu ya kuwepo kwa elimu hiyo, mahali na muda itakayokuwa ikitolewa ili watu wengi waweze kuhudhuria.

(iv) Ikiwezekana njia mojawapo ya kutoa matangazo na elimu iwe kwa njia ya vipeperushi.

Katika Kifungu cha (8) kinachozungumzia kujiandikisha kuwa ni wakati wa uchaguzi au kabla waliofikia umri wa miaka 18 kujiandikisha. Hivi karibuni kumetolewa matangazo kupitia vyombo vya habari hususani magazeti kwamba uandikishaji utafanyika Kimkoa au Kanda na muda umewekwa. Je, baada ya muda huu kupita uandikishaji Kikanda wale waliofikia miaka 18 wataendelea kujiandikisha? Mimi nashauri waendelee kujiandikisha.

Katika Kifungu (9) kinachozungumzia Tume ya Uchaguzi kuweza kuwa na Daftari la Wapiga Kura la Muda katika kutayarisha Daftari la Wapiga Kura la Kudumu kwa ajili ya:-

- Ukaguzi;
- Kufanya mabadiliko ya makazi;
- Kupinga uandikishaji;
- Kuingiza au kutoa majina ya wapiga kura;
- Kufanya marekebisho.

Badala ya kuwa na Daftari la Muda kwanza kisha kuwa na Daftari la Kudumu nashauri kazi zinazoonyeshwa katika Daftari la Muda liwe la Kudumu kwa sababu:-

(a) Vifo vinatokea kila mara;
(b) Watoto wanazaliwa kila siku na wanaotimiza miaka 18 wapo kila siku;
(c) Watu wanabadilisha makazi kila mara kutokana na sababu mbalimbali;
(d) Watu kama wafanyakazi wanahamishwa kila mara.

Kwa hiyo, kazi zinazoonyeshwa katika Daftari la Muda zitakuwa ni za kudumu kutokana na sababu nilizozieleza.

Katiba Kifungu cha 13 ambacho kinazungumzia wajibu wa Tume wa kupanga muda wa kuhuisha Daftari la Wapiga Kura. Hapa nashauri kazi hii ipewe muda wa kutosha au iwe ni kazi ya kudumu kuwezesha watendaji kuifanya kwa ufanisi. Isipofanywa hivyo na kupanga muda mfupi usiotosha kutafanya kazi hiyo kufanyika kwa fujo na vurugu hasa kama itafanywa wakati wa uchaguzi

Katika vifungu vinavyozungumzia masuala ya rufaa, maelekezo ni kwamba kazi hii inatakiwa kufanywa na Mahakama za Wilaya na kwamba muda wa kuamua mashauri hayo ni siku kati ya saba na siku kumi na nne. Muda huu unatolewa kama vile hizi Mahakama zitakuwa hazina kazi nyingine isipokuwa ni hizo. Lakini kuna wakata rufaa wengine wanataka kutumia Mawakili na uzoefu unaonyesha kuwa kutumia Mawakili huchukua muda mrefu kwa sababu wana kazi nyingi. Hivi kama shauri litakuwa halijaisha itakuwaje? Naomba hilo litazamwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja lakini ningependa nifafanuliwe kuhusu uandikishwaji wa wapiga kura kwenye daftari.

Kwa miji ya Pwani yaani Dar es Salaam, Bagamoyo, Tanga kumejitokeza uhamiaji wa wananchi kutoka Pemba. Hawa wanatarajia kujiandikisha kama raia wengine. Tatizo ni kwamba wananchi wa kutoka Bara wakitaka kupiga kura Zanzibar, hukataliwa isipokuwa kama wataonyesha ushahidi kuwa wameishi Zanzibar kwa kipindi kisichopungua miaka 10 na Waziri wa Tawala za Mikoa kule hutoa *Certificate* kuthibitisha hilo. Sasa basi huku Bara hawa wananchi wengi kutoka Pemba huwa wanaruhusiwa kupiga kura bila ya kujali wameishi muda gani huku Bara. Hii siyo sahihi. Hivyo basi nao Wapemba wasiruhusiwe kuandikishwa mpaka waonyeshe kuwa wameishi miaka 10 huku Bara. Wananchi wa Dar es Salaam wao wangependa uchaguzi wao usiwajumuishe hawa Wapemba warudi kwao kupiga kura wanatuletea taabu tu. Sasa hivi wamenunua nusu ya nyumba za Ilala na kila nyumba ina watu wanaoishi humo wasiopungua ishirini. Hawa wakipiga kura watatuletea shida tu. Misimamo yao si ya ki-Bara

Mheshimiwa Spika, Daftari hili lizingatiwe haya matatizo ya Upemba na Ubara.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi, naunga mkono marekebisho yote yaliyofanyika. Naamini kuwa kama zoezi la kuwa na Daftari la Wapiga Kura likikamilika itasaidia kupunguza gharama za uchaguzi pia malalamiko mbalimbali yaliyotokana na utaratibu wa zamani ama wa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, hapa nina tatizo moja tu naomba nifahamu. Kata ya Liuli Wilayani Mbinga haina Diwani kuanzia mwishoni mwa mwaka jana na hadi hii leo uchaguzi mdogo haujatangazwa na Tume ya Uchaguzi, haifahamiki ni nini kinachokwamisha uchaguzi usifanyike katika Kata hii ya Liuli?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono Muswada huu kwa mara ya pili.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sikusudii kumwita mtoa hoja kwa sababu michango mingi imetolewa, inahitaji majibu nafikiri ni vizuri tukampa nafasi akaandaa majibu yake vizuri, akawasiliana na wataalam wake ili majibu yatakayotoka yawe yanafanana na uzito wa Bunge hili. Kwa hiyo, napenda kipindi cha asubuhi kiishie hapa

na tumwite mtoa hoja tutakaporejea saa 11.00 jioni, halafu tutaendelea na hatua za kukamilisha Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.06 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii kumalizia Muswada ambao niliuwasilisha asubuhi. Kwanza ningependa niwatambue wale ambao wamechangia hoja hii kabla ya kuanza kujumlisha masuala mbalimbali ambayo Wabunge walichangia. Waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Athuman Janguo, ambaye ni Mbunge wa Kisarawe na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, akifuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga Makongoro, Mbunge wa Ukonga, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ali, Mbunge wa Kwahani, Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa na Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni; Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi na Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa niruhusu nianze kujibu hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Kwanza ningependa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi, kuchangia kwa kuzungumza na pia wale ambao walikuwa Bungeni hapa kwa muda wote kusikiliza hoja hii kwa sababu kama wasingekuwepo basi *quorum* isingetimia. Kwa hiyo, nawashukuru wote ambao wamehudhuria asubuhi na jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo nitalianza ni ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga. Yeye alisema kwamba kuna haja Serikali kuweka Mahakama maalum ya kujadili malalamiko ya uchaguzi. Serikali inaona kwamba jambo hili halina msingi wowote kwa sababu tayari kuna Sheria ya Uchaguzi Kifungu Namba 115 ambacho kimeweka muda maalum kwamba lazima kesi zote zimalizike. Kwa hiyo, nafikiri kwa sasa hivi ni gharama za bure na bado tunahitaji Mahakimu hawa na Majaji kwa ajili ya kesi nyingine muhimu zaidi kuliko hizi. Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiri kwamba kwa kuwa kifungu hiki kipo na kinatoa masharti kwamba lazima kesi hizo za uchaguzi zimalizike kwa muda mfupi na zitamalizika.

Lakini pia utaratibu huu wa kuanzisha Daftari la Kudumu pia litasaidia kupunguza malalamiko mengi kwa wananchi kuhusu uchaguzi. Kwa hiyo, tunafikiri hiyo haina haja kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Mheshimiwa Mutungirehi alizungumza kwamba hakuna haja ya wagombea Urais na Makamu wa Rais kula kiapo wakati wa kuwakilisha nyaraka zao. Nashukuru Mheshimiwa Shellukindo kasaidia sana kwa sababu ni muhimu sana kwa sababu anatakiwa yule ambaye anaomba Urais au Makamu wa Rais awe Mtakatifu kweli kweli, asidanganye Taifa hili. Kwa hiyo, ndiyo maana tunaweka siku maalum wanakwenda kula kiapo pale kuthibitisha yale yote waliyosema ni kweli na endapo atakuwa hakusema kweli anaweza kupingwa kabla ya uchaguzi kuanza. Nafikiri hii ni muhimu sana kwa ajili ya uwazi na ukweli na pia kujenga maadili mazuri kwa nchi yetu. Nafikiri bado kuna umuhimu wa kwenda kula kiapo, kama mtu anasema ana *degree* tatu zionekane ni tatu kweli, kama ziko nne, ziwe nne kweli, kapata wapi na kadhalika. Hawezi kuwa mtu awe na *degree* ya kwanza halafu hakusoma *form four* wala *high school* hakufika lakini ana *degree* tena kwa mwaka mmoja, kwa mfano mwakani Oktoba mtu anapata *degree,* hiyo haiwezekani na yatakuwa mambo ya ajabu kabisa. Kwa hiyo, nafikiri ni muhimu Waheshimiwa Wabunge turuhusu hawa watu wakale kiapo mbele ya Majaji ili wathibitishe kwamba wanayosema ni kweli na ni Watakatifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililozungumziwa ni la wapiga kura wa uchaguzi wa Rais. Wamesema kwamba kuna ubaguzi, lakini nafikiri hakuna ubaguzi, la msingi ni kwamba Jimbo la Rais ni Tanzania nzima bara na visiwani. Popote pale Mtanzania alipo ana haki ya kupiga kura ya Rais wa Tanzania. Lakini si vizuri pia kuruhusu kila mtu apige kura katika Jimbo ambalo yeye hakai pale, hasa kwa Zanzibar ambayo ni nchi ndogo sana. Inawezekana mtu akaona kwamba uchaguzi ujao atashindwa basi anasema naomba nijaze majahazi kama kumi kutoka bara yaje kunisaidia kwenye Jimbo langu ili ashinde pale kura ya Ubunge au Uwakilishi. Kwa hiyo, ni muhimu kuweka *restriction* kwamba Jimbo la Rais ni nchi nzima lakini kwa Wabunge au Wawakilishi wa Zanzibar ni wale ambao wakazi wa pale na ndivyo sheria inavyosema. Kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wabunge walielewe na kulikubali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili lililozungumziwa ni ushirikiano wa Tume na Vyama vya Siasa. Tunakubali kuwa ni muhimu sana kuwepo na ushirikiano katika ngazi za Taifa, Wilaya na katika Jimbo ili kufanya uchaguzi huu uwe mzuri na halali kabisa, hilo tunakubaliana nalo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililozungumzwa ni la Tume huru. Nashukuru kwamba Dr. Slaa ametusaidia sana kuelezea kwamba yeye ana imani kubwa sana na Tume ya Uchaguzi Tanzania na ametuambia huko nje pia wanaisifu Tume hii ya Uchaguzi ya Tanzania. Kwa hiyo, sisi wenyewe tusiiponde Tume yetu wakati watu wa nje wanaisifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kwamba Tume hii imechaguliwa na Rais, kwa hiyo itampendelea Rais si kweli hata kidogo kwa sababu kuna masharti ya Katiba

yaliyokataza kwamba Tume isifuate maelekezo ya mtu yeyote au ya Chama chochote katika nchi hii. Kwa hiyo, wao wanafuata maelekezo hayo kwa hiyo kuchaguliwa na Rais si tatizo kwa sababu ninyi hapa mnajua kwamba Mheshimiwa Hamad Rashid kachaguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na yeye yupo *CUF.* Lakini si lazima amwunge mkono Rais, hapa anapinga tu kwa sababu ana uhuru kabisa. Hata Zanzibar kule kuna Wawakilishi wawili wa Chama cha *CUF* katika Baraza la Wawakilishi ni bwana Masoud na Havijali.

**MBUNGE FULANI:** Ni mmoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Hata huyo huyo mmoja, lakini yeye halazimishwi kuunga mkono Chama cha Mapinduzi Zanzibar kule kwa sababu ana uhuru kabisa. Kwa hiyo, kuchaguliwa haitoshi lazima ufuate maadili na hii Tume ya Uchaguzi ina maadili yake, sheria zake na taratibu zake. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba tusiwaogope hawa jamaa, wale wanatusaidia sana na kweli namshukuru Dr. Slaa na ningependa awaelimishe wenzake kwamba kweli Tume hii inajitahidi sana, tuisaidie ifanye kazi kwa busara zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, kulikuwa na maelezo hapa kwamba anayejitoa katika Ubunge basi afungwe miaka arobaini, enhee. Atakayesema anajitoa katika kugombea Ubunge basi adhabu yake afungwe miaka arobaini, mambo makubwa sana hayo. Naomba tusiwe na jazba katika mambo haya, mtu akiona maji mazito anatoka tu anaacha wengine wanaelea tu. *(Makofi)*

Mgombea ana haki ya msingi ya kugombea na ana haki ya kujitoa, cha muhimu ni kufuata taratibu tu. Mimi nafikiri tusiwatishe watu ambao wanataka kujitoa katika Vyama vyetu kwa sababu ya kuogopa, tuwaache waende katika uchaguzi wakiona kwamba hali haiwezekani wanajitoa, anakuja mwingine na kadhalika. Kwa hiyo, nafikiri hakuna haja ya kuwaadhibu watu na kwa kweli si demokrasia hiyo kumfunga mtu miaka arobaini kwa kujitoa katika kugombea Ubunge wa Jimbo fulani. Hapa tungewafunga wengi sana, wengi wametoka, kwa hiyo hili halina haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililozungumzwa ni juu ya elimu ya wapiga kura. Tume yetu jukumu lake kubwa ni kuratibu na kusimamia zaidi na kwa hiyo itaratibu pia *NGOs* zote ambazo zinafanya hii elimu ya wapiga kura. Ni muhimu kwa sababu wao wanajua kwamba ni mambo gani yazungumzwe, kama kuna matatizo wataambiwa, badala ya kutumia tu *NGOs* kupigia debe Chama kimoja au kingine. Kwa hiyo, Tume ya Uchaguzi ndiyo ina mamlaka ya kisheria kuona kwamba yanayozungumzwa katika elimu hii ni yale ambayo yanakubalika Kitaifa na kimaadili. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono jambo hili ambalo ni zuri sana kwa ajili ya uchaguzi nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limezungumzwa suala la wagonjwa na wazee kwamba Tume ifanye utaratibu wa kuwafuata huko walipo. Nafikiri hii ni kazi kubwa sana. Hiyo ni kazi ya Vyama vya Siasa vyenyewe na wenyewe waliokuwa wagonjwa na

watu wazima. Linaweza kufanyika muda wowote hakuna tatizo lolote. Kwa hiyo, nafikiri kwamba haina haja Tume kupewa kazi ya kufuatilia wagonjwa waliopo huko na kuwapa amri sijui ya kupiga kura, utakuwa na kazi ngapi na watu wangapi watafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, hii kazi tuwaachie wananchi na viongozi wenyewe wa Vyama vya Siasa na linafanyika hili mara nyingi sana, kama mkiona mzee anakuja pale au mgonjwa mnampa nafasi na hili linafanyika, si jambo geni kwetu sisi. Kwa hiyo, ningeomba hili tuliache.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililozungumziwa ni juu ya wale ambao wanaishi nje ya nchi waruhusiwe kupiga kura hapa nyumbani ya Urais na Ubunge na Uwakilishi. Tunafikiri jambo hili kwa sasa si busara labda siku zijazo kwa sababu unaweza ukachukua kundi la watu nje ambao labda walikimbia nchi, ukawaleta hapa wakaharibu mambo yote, hawajui sera zetu, hawajui mwenendo wetu, wako nje waje tu kupiga kura basi. Kwa hiyo, nafikiri hili si muhimu kwa sasa hivi, naomba tuliache. Sisi ambao tunatoka Zanzibar tunajua kwamba watu wengi sana wapo nje kule, kwa hiyo wakija kiasi cha watu elfu moja, basi tayari wameshabadilisha mwelekeo wa kura. Kwa hiyo, ni vizuri nafikiri tusubiri kwanza mpaka hapo baadaye na zile nchi ambazo zinafanya hivi pia zina matatizo makubwa sana. Labda tutajaribu hapo baadaye lakini kwa sasa hivi tuache kwanza, Watanzania aliye ndani ya Tanzania ndiyo wapige kura, wale walio nje wasubiri siku za mbele wataweza kufanya hivyo. Nafikiri hili tuliunge mkono kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa kwamba daftari la wapiga kura halifahamiki kwa watu wengi, inaweza kuwa ni kweli lakini Tume imeandaa ratiba maalum ambayo itawaelimisha wananchi na wapiga kura. Tulianza kuwaelimisha viongozi wa Vyama vya Siasa, lakini wakakimbia kwenye mkutano ule, lakini tutaendelea, tutawaita tena viongozi mara ya pili tuwaelimishe, tunakusudia pia kuweka semina hapa Bungeni kwa ajili ya Wabunge ili kuelimisha juu ya jambo hili na ninyi kama wawakilishi wa wananchi mtasaidia kuwaelimisha wananchi wetu juu ya Daftari la Kudumu la wapiga kura. Kwa hiyo, tutafanya kazi hii na naomba msaidie hapo wakati utakapofika kuwaelimisha wananchi wengine kuhusu daftari hili la wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshauriwa kwamba tuwe na orodha ya wapiga kura iwe katika *computer*. Hili linazingatiwa na ni zuri sana halina ubaya wowote ule. Lakini kusema kwamba haiwezekani mtu akaweza ku-*temper* haya majina kuwa vingine, haiwezekani. Kuna Mbunge mmoja alisema inawezekana mtu akaja akatumia teknolojia zake akapunguza, haiwezekani, tutajitahidi sana kuzuia mtu asiweze kupotosha takwimu hizi, kwa hiyo kutakuwa na uangalizi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Slaa alizungumza hapa kuhusu vitambulisho. Alitaka tuseme kwamba lini vitambulisho vitatoka, jibu lake ni kwamba vitambulisho haviwezi kutoka kabla ya uchaguzi, kati ya leo na Oktoba haiwezekani kwa sababu hatuna muda huo wa vitambulisho. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wasubiri mpaka hapo Serikali itakapotoa vitambulisho hivi. Lakini mjue kwamba miaka mingi tumefanya uchaguzi bila vitambulisho huu siouchaguzi wa kwanza. Kwa hiyo, si jambo geni kufanya uchaguzi bila vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua umuhimu wake lakini tunajua kwamba katika utaratibu wetu huu wa kupiga kura kuna pingamizi, kwa hiyo endapo ukimwona mtu katika Daftari la Wapiga kura ambaye si raia au hana haki unaweza kupinga, kuna siku maalum ambayo watawekwa kwenye ukuta watu wote ambao ni wapiga kura. Kwa hiyo, inawezekana kabisa na bila shaka Vyama vya Siasa ambavyo ni mahiri havitakubali kuona kwamba mpiga kura ambaye hana haki anapiga kura, lazima watampinga tu, ndiyo maana ya kuweka katika *display*. Kwa hiyo, ningeomba kwamba Viongozi wetu wa Vyama vya Siasa, wale ambao wanafikiri si raia basi wawapinge ili wasipate haki ambayo si yao. Lakini pia katika nchi yetu tuna viongozi wa Vijiji na Kata ambao pia wanawajua watu wanaokaa katika maeneo yao hasa mpakani kule. Kwa hiyo, nafikiri kazi hii ni yetu sote, wakati tunasubiri vitambulisho vya uraia basi Vyama vya Siasa na viongozi tusaidiane katika kuwabaini wale ambao tunafikiri kwamba hawana haki ya kupiga kura katika nchi yetu. Kuna hofu kwamba muda uliobaki kati ya leo na Oktoba mwakani Daftari hili halitaweza kufanikiwa, si kweli. Tumeanza kazi hii toka mwaka 2001 na ninaamini kwamba ifikapo Oktoba mwakani kila kitu kitakuwa tayari na watu watapiga kura kwa usalama zaidi. Kwa hiyo, tunaomba mtuamini kwamba inawezekana kufanya hivi kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine ambayo imezungumzwa sana hapa kuhusu watendaji wa Halmashauri. Nashukuru kwamba Dr. Slaa, amenisaidia kwa kusema kwamba yeye hana mashaka nayo. Ni kweli kwamba siku za nyuma mwaka 1995, Serikali ilijaribu kuwachukua watu mitaani huko wastaafu, walimu, wanafunzi kuwapa kazi hii matokeo yake kulikuwa na vurugu kubwa sana na kesi nyingi sana zilikuwa za uchaguzi wa mwaka 1995. Kwa hiyo tunafikiri kwamba ni vema kumpa kazi mtu ambaye unaweza kumdhibiti akifanya makosa na ili kuthibitisha hayo tumeweka sheria hapa kwamba endapo utaona kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri amefanya makosa kwa kukusudia basi kuna adhabu ya kifungo cha miaka miwili au faini ya shilingi milioni mbili si kidogo hizo. Lakini wewe pia mwananchi wa kawaida ukiona kwamba huyu Mkurugenzi ambaye anataka kupewa kazi hii unaweza kuweka pingamizi kwa Tume ya Uchaguzi. Kwa hiyo, kuna vipengele mbalimbali katika kudhibiti hali hii.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Waheshimiwa Wabunge watuamini kwamba zoezi ni muhimu sana, lazima wapewe watu makini, wenye busara, hekima na pia unaoweza kuwaadhibu endapo watafanya makosa na kuzembea katika jambo hili. Pia hawa wanakula kiapo mbele ya wahusika na zipo adhabu za kuwaadhibu. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge watuamini, hili suala la kwamba hawa wapo chini ya Waziri wa Tawala za Mikoa halina msingi hata kidogo. Mwanzo nimetoa mfano kwamba Rais pia anateua wengi tu Majaji na kadhalika na hawamfuati yeye, wanafuata sheria, taratibu na kanuni. Kwa hiyo, hawa Wakurugenzi wa Halmashauri wanafuata taratibu, kanuni na sheria ambazo zinawaongoza. Ningeomba hilo pia Waheshimiwa Wabunge watuamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daftari hili ni muhimu sana na tunalileta kwenu ninyi ili kuitikia wito wa Katiba kwani Katiba yetu imetaka tuwe na Daftari la Kudumu, tumechelewa sana. Kwa hiyo, tumeleta kwenu ninyi tunaomba mtuunge mkono ili

tutekeleze maelekezo ya Katiba yetu kwamba kutakuwa na Daftari la kudumu. Lakini hapa kulikuwa na mawazo tofauti, Dr. Mahanga alisema kwamba Serikali imeshurutishwa na wafadhili, naye Mheshimiwa Lwakatare anasema kwamba Daftari hili limeshinikizwa na Kambi ya Upinzani. Yote si kweli, sisi hatuongozwi na wapinzani wala wafadhili, tunaongozwa na sera zetu za Chama cha Mapinduzi na nyie mnajua kwamba sera yetu ni uwazi na ukweli. Ndiyo Daftari hili linajibu hoja hiyo kwamba tunataka kazi iwe wazi na kweli, kila mtu aone kinafanyika nini, kwa hiyo si kweli kwamba tumeelekezwa na wafadhili au na Wapinzani. Si vibaya, kama kuna hoja nzuri ya Wapinzani Serikali inaichukua tu au kuna hoja nzuri ya wafadhili tunaichukua tu lakini hatulazimishwi hata kidogo. Kwa hiyo, ningeomba Waheshimiwa Wabunge tujipe heshima wenyewe kwamba haya ni mambo yetu wenyewe, mambo ya Chama cha Mapinduzi. Au kuna mtu anabisha hilo, hakuna anayebisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, faida za Daftari zipo nyingi sana, nitaeleza machache tu. Kwanza shahada zote zitakuwa na picha ya mpiga kura, picha ambayo itapigwa na Tume ya Uchaguzi siyo ya nyumbani kwako. Kutakuwa na saini yako katika kitambulisho chako. Kutakuwana dole gumba lako ambalo unaweka pale. Kwa hiyo, ni vigumu kuiba kura sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili litazuia mtindo wa watu kununua shahada za kura, kuna mtindo wa watu kununua shahada, kwa sasa hivi mtindo huo hautakuwepo kwa sababu kila mtu kuna sura yake. Litazuia mtu kupiga kura zaidi ya mara moja. Litazuia watu kuchukua watu wa Tanga kuwapeleka Unguja au Pemba kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia linapunguza sana gharama ya kuendesha uchaguzi kila baada ya miaka mitano kwa sababu Daftari linabaki pale, wewe unapunguza waliokufa na unaongeza waliofikisha umri wa kupiga kura. Kwa hiyo, pia linapunguza gharama na fedha hizo zitatumika kwa ajili ya matumizi mengine ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, nafikiri kwamba jambo hili ni muhimu sana naomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono. Pia litaimarisha uwazi, uhuru, haki na demokrasia katika uchaguzi wetu, mtu akishinda anashinda kihalali.

Wakati wa asubuhi Mheshimiwa Janguo aliwasilisha hapa maelezo ya Kamati si vizuri kutomshukuru, napenda nimshukuru sana kwa kuwasilisha waraka wake lakini kusaidia Kamati yetu kwa hekima na uadilifu mkubwa sana kwa vipindi vyote vile ambavyo tumekaa naye.

Lakini busara zaidi ameitumia wakati wa wadau, viongozi wa Vyama vya Upinzani pale Dar es Salaam hasa Wenyeviti ambao wote walikuwepo na alifanya kazi kubwa sana kuwashawishi wazungumzie hoja badala ya malumbano. Lakini kama ilivyo kawaida wengine wakacharuka, bahati mbaya akiwemo Bwana Chipaka, Bwana Makaidi na Bwana Mtikila. Kwa hiyo, busara ya Mzee Janguo hapa haikufua dafu. Lakini si ajabu, Waswahili wanasema kwamba jina zuri mpe mwanao, sasa mtoto umempa jina la Chipaka au Mkaidi. *(Kicheko)*

Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wengine pale pale walikuwa na busara wakasikiliza kwa makini akina Lipumba na wenzake, CCM walikuwepo pia. Lakini wengine wakacharuka, lakini huyu Chipaka na Makaidi utawafanya nini, unawaacha tu. Kwa hiyo, wakati mwingine ni vizuri kujenga hoja ya kuzungumza sio kutoa mapovu tu. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Janguo umetusaidia sana kuweka sawasawa tukafanikiwa kuzungumza na maoni yao wengi Wapinzani tumeyaingiza kwa sababu siyo kwenda safarini na jahazi moja tu lazima tujenge ushirikiano.

Maagizo ya Kamati yalikuwa, moja ni kwamba tutekeleze yote waliyotuambia, mmeona kuna masahihisho mengi tu humu. Lakini pia wametutaka tuwe makini katika kufuatilia wale ambao umri wao umefika, wawe na vitambulisho kama kweli hawa umri wao umetimia kupiga kura. Pia wamesema kwamba tujitahidi kudhibiti hawa maafisa ambao watafanya uzembe. Nafikiri hayo ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nichukue nafasi hii kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Abdallah Kigoda na ndugu yake kwa msiba uliowafika na Mungu ajaalie roho ya marehemu iwe mahali pema, *Inshallah.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa sababu Wabunge wote wameunga mkono nimalizie kwa kusema kwamba, nampongeza sana Mheshimiwa Makanga kwa ushindi wake wa kishindo. *(Makofi)*

Jambo moja ambalo si la kawaida kwa Mheshimiwa Makanga ni kutofuata itifaki, maana yake wanasema itifaki izingatiwe, yeye hakufuata itifaki, kwa vipi? Kwanza, kamwangusha bosi wake wa zamani. Hawezi kuwa bosi wako halafu ukamwangusha kwenye uchaguzi na ambaye ni Mwenyekiti wako wa zamani pia na akatumia stahili ile ile *out,* tukampiga *out* na yeye huku. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia amemshinda mtu ambaye mara nyingi kagombea Urais pia kashindwa na zaidi kambwaga nyumbani kwake. Kwa hiyo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa jitihada yake hiyo ya kumwangusha bosi wake wa zamani. Mimi nisingeweza kumwangusha Waziri Mkuu Jimboni kwake hata kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba Waheshimiwa Wabunge sasa hivi muunge mkono hoja yangu hii ili tuimarishe Daftari hili, tuwasubiri wataalam waanze kazi ili litusaidie kwa ajili ya uchaguzi wa mwakani. Mimi naamini kwamba mwakani watakaoingia hapa watakuwa ni viongozi halali hawakuibiwa kura kwa sababu Daftari litakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria za Uchaguzi wa Mwaka 2004**
***(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Muswada huu una vifungu sitini na saba kwa kupitia kifungu kwa kifungu nitawahoji mara sitini na saba. Sasa nafikiri tutahoji kwa kupitia sehemu kwa sehemu na *amendments* zote zitatajwa. Kwa mtu yeyote mwenye hoja katika sehemu yoyote anaweza kusimama ili nimpatie nafasi. Endelea Katibu.

Sehemu ya 1

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya BungeZima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 2
Sehemu ya 3

*(Sehemu zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria za Uchaguzi wa Mwaka 2004**
***(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi *(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004)* kifungu kwa kifungu na kuukubali. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge shughuli tulizokuwa nazo jioni hii tumeishia hapo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.28 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 10 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*